



Mshiriki wa Mradi wa Majaribio



Lifeboats



Mradi wa Usalama Majini  
Mwongozo

# Kuhusu muongozo huu

Lengo la msingi la Mradi wa Usalama Majini ni kuokoa maisha kwa kuwafundisha watu mambo muhimu ya usalama wa majini na inapowezekana, kuwapa ujuzi wa msingi wa kujiokoa majini.

Mradi huu umewalenga vijana wanaoishi katika maeneo yenye nyenzo duni na zisizokuwa na huduma za kuzuia kuzama na kufa maji.

Imetengenezwa kusaidia mashirika na watu binafsi kutekeleza Mradi wa Usalama Majini kama sehemu ya mkakati wa kienyeji au kitaifa wa kuzuia uzamaji.

Mwongozo huu umebuniwa kama hati ya uongozi na inaweza kubadilishwa kulingana na mazingira husika. Ambapo imewezezana hati hii imeingiza njia bora zilizobuniwa na mashirika ya kuzuia uzamaji.

## Rasimu ya 3.0:

Disemba 2015

Zimejaribiwa na kutengenezwa na:



Royal National Lifeboat Institution  
West Quay Road  
Poole  
Dorset  
BH15 1HZ  
England

Simu: +44 (0) 1202 663000  
Mtandao: [www.rnli.org.uk/international](http://www.rnli.org.uk/international)  
Barua pepe: [international@rnli.org.uk](mailto:international@rnli.org.uk)

Kwa maswali ya kiufundi au maelezo zaidi tafadhali wasiliana na RNLI kupitia [international@rnli.org.uk](mailto:international@rnli.org.uk).

RNLI imesajiliwa kama shirika la kujitolea nchini Uengereza na Wales (209603) na Scotland (SC037736). Namba ya usajili CHY 2678 huko Jamhuri ya Ireland.

Hati hii inaweza kuchapiswa tena bila ya ridhaa ya RNLI. RNLI haichukui jukumu lolote kwa matokeo yalosababishwa na mwongozo huu.

Picha:

RNLI/Mike Lavis, Nile Swimmers

Msaada wa kiufundi ultolewa na:



Onyo

Maudhui ya mwongozo huu ni kwa ajili ya uongozi wa jumla tu. Inawakilisha njia bora kwa tarehe ya uchapishaji na haipaswi kutumika kama ushauri wa kisheria. Watumiaji wa muongozo huu lazima watafute ushauri wa kitaalamu inapobidi. RNLI haichukui jukumu lolote kwa makosa yalokuwemo kwenye hati hii.

# Contents

<b>Utangulizi</b>	<b>4</b>
<b>Kuzama na jukumu la Mradi wa Usalama Majini</b>	<b>5</b>
<b>Kufahamu mchakato wa kuzama</b>	<b>5</b>
Kwa nini watu wanazama.....	6
Kujua tatizo .....	7
Ambao wanaweza kuzama.....	7
Makundi yaliyo hatarini .....	8
<b>Mradi wa Usalama Majini</b>	<b>10</b>
Nini jukumu la Mradi wa Usalama Majini? .....	10
Sehemu ya 1: Elimu kwa Jamii - Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini.....	10
Sehemu ya 2: Kujiokoa na Kuokoa .....	10
Nija za Kupeleka Ujumbe .....	11
1. Ujumbe kwa Jamii .....	11
2. Ujumbe kwa Walengwa.....	11
Fedha 1.1.....	11
Ada ya Mafunzo.....	11
Ruzuku.....	11
Michango ya jamii .....	11
<b>Sehemu ya 1:</b>	
<b>    Elemu kwa Jamii - Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini</b>	<b>12</b>
<b>1.1 Mipango na maandalizi</b>	<b>13</b>
Kwa nini uendeshe Mradi wa Elimu kwa Jamii?.....	13
Wasikilizaji.....	13
Ufikishajji.....	14
Mkutano wa wadau .....	14
Zana .....	15
Walimu .....	15
Eneo .....	16
<b>1.2 Kufundisha ujumbe</b>	<b>17</b>
Ujumbe wa usalama majini.....	17
Jinsi ya kufundisha ujumbe.....	18
<b>1.3 Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini - Mpangilio wa somo</b>	<b>19</b>
Flash cards – Mandhari.....	21
Itambue hatari .....	21
Jiweke salama .....	29
Waweke wengine salama.....	39

# Contents

<b>Sehemu ya 2: Kujiokoa na Uokoaji</b>	<b>47</b>
<b>2.1 Mipango na maandalizi</b>	<b>48</b>
Vitendea Kazi.....	48
Muda.....	49
Walimu .....	49
Kuchagua sehemu salama ya kufundishia kugoelea.....	49
Kukagua eneo la la kufundishia.....	52
Eneo la kuogelea - orodha ya ukaguzi .....	53
Kutaarisha eneo la kufundishia.....	54
Vifaa vya kufundishia.....	55
<b>2.2 Maandalizi ya somo</b>	<b>56</b>
Usalama wa mwalimu.....	56
Mavazi sahihi .....	56
Usalama juani.....	57
Usalama wa wanafunzi.....	58
Kufanya eneo la kufundishia kuwa salama.....	59
Mavazi sahihi .....	59
Hali ya kiafya .....	59
Msaada .....	59
Maandalizi ya darasa.....	60
Ukubwa wa darasa.....	60
Kuwagawa wanafunzi.....	61
Maandalizi na usalama orodha ya ukaguzi.....	62
<b>2.3 Usimamizi wa</b>	<b>63</b>
Kuweka sheria .....	63
Kanuni za nidhamu.....	63
Kuweka matarajio .....	64
Desturi .....	64
Motisha .....	64
Kujiweka .....	65
Mazoezi.....	65
Mfumo wa wawili wawili.....	65
Mifano .....	66
<b>2.4 Ujuzi wa uokuaji kwa walimu</b>	<b>67</b>
Kupata msaada.....	67
Wapeleke wanafunzi eneo salama.....	68
Anzisha mawasiliano ya sauti.....	68
Aina za uokozi .....	68
Uokoaji wa nchi kavu.....	69
Uokozi wa kumfikia.....	69
Uokozi wa kurusha.....	70
Uokozi wa kujwamua.....	71
Uokozi wa kuogelea.....	72
1. Kuingia majini .....	72
2. Kuogelea kwenda kwa mtu aliye matatizoni.....	72
3. Kumkaribia mtu aliye matatizoni.....	73
4. Kumrudisha muhusika ufukweni.....	73

# Contents

<b>2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu</b>	<b>75</b>
Huduma ya kwanza ni nini?.....	75
Kanuni za huduma ya kwanza.....	75
Tathmini .....	76
Tafuta chanzo cha hatari.....	76
Angalia njia ya hewa .....	76
Kama mtu amepoteza fahamu.....	76
Angalia njia ya hewa.....	76
Angalia upumuaji.....	76
Cha kufanya akianza kutapika.....	76
Kama muhusika anapumua kikawaida.....	77
Mkao wa kupona .....	77
Kama muhusika hapumui kikawaida .....	78
Ufunguaji wa njia za hewa na upumuaji wa awali.....	78
Angalia dalili za uhai (Mzunguko) .....	78
Kama hakuna dalili za uhai.....	79
Ukandamizaji wa kifua.....	79
Kama mtu hajapoteza fahamu.....	80
Majeraha.....	80
Mifupa iliyovunjika.....	81
Uvujaji wa damu puan.....	81
Kutafunwa na mnyama.....	82
<b>2.6 Mahitaji ya kufundishia</b>	<b>83</b>
Ujuzi wa msingi.....	83
Maandalizi .....	83
Mapigo.....	83
Msaada.....	83
Kufundisha ujuzi wa msingi.....	84
Maendeleo.....	84
Usajili .....	84
Tathmini .....	84
Ratiba ya somo .....	85
Fomu ya mahudhirio na tathmini .....	86
<b>2.7 Mpangilio wa somo</b>	<b>87</b>
Somo 1–12 .....	87–147
Maandalizi	
Mapigo	
Msaada	
Mazoezi	
Somo la 13.....	148
Mazoezi	
Tathmini	
<b>2.8 Michezo na Vitendo</b>	<b>149</b>

# Utangulizi



Wengi wetu hutumia maji kila siku kwa ajili ya kuoga, kusafisha, shughuli za burudani na usafiri.

Katika maeneo yenye nyenzo za kutosha, shughuli hizi hufanywa katika mazingira salama ya nyumbani, au katika maeneo yanayosimamiwa ipasavyo. Katika maeneo yenye nyenzo duni, watu wengi hawana chaguo bali kufanya shughuli hizi muhimu katika maeneo ya wazi licha ya kujua hatari zake. Usafiri wa majini kwa ujumla hauna udhibiti, na vyombo mara nyingi huwa havina vifaa vya kutosha vya usalama.

Kuanguka majini ni hatari, na matokeo yake yanaweza kuwa mabaya - hasa kama mtu hawezi kuogelea au kuokolewa.

Kuogolea kwa kawaida huwa si sehemu ya elimu rasmi na kwa ujumla maelezo ya jinsi ya kuwa salama ndani na pembezoni mwa maji hayapatikani.

Royal National Lifeboat Institution (RNLI) na jumuia washiriki wametengeneza Mradi wa Usalama Majini, maalum kwa matumizi ya maeneo yenye nyenzo duni. Mwongozo huu ni rahisi lakini ni muongozo muhimu kwa mashirika yanayotaka kutumia mradi huu.

# Kuzama na jukumu la Mradi wa Usalama Majini



Matokeo ya kujifunza:

1. Kufahamu mchakato wa kuzama.
2. Kufahamu kwa nini watu wanazama.
3. Kufahamu nani mwenye uwezekano wa kuzama.

## Kufahamu mchakato wa kuzama.

Karibia 70% ya uso wa dunia umefunikwa na maji. Maji hutumika kwa shughuli nyingi za kila siku kama vile burudani, kuoga, uoshaji, uvuvi na usafiri.

Katika maeneo yenye nyenzo za kutosha, matumizi ya maji kwa ujumla hufanyika katika mazingira salama ya nyumbani au katika maeneo yanayosimamiwa. Hata hivyo katika maeneo yenye nyenzo duni, watu wengi hutumia vyanzo vya maji vilivyowazi kama vile maziwa, mito na bahari kutekeleza shughuli hizo.

kuanguka majini ni hatari na majanga yake yanaweza kuwa makubwa hasa kama mtu atashindwa kuogelea au kuokolewa.


Kuzama hutokea pale mtu anaposhindwa kupumua kwa sababu kichwa chake kimefunkwa na maji.



# Kufahamu mchakato wa kuzama

## 1.2 Kwa nini watu wanazama

Hali inayoruhusu uzamaji inaweza kuelezewa kwa mukhtasari unaoitwa Mnyororo wa Kuzama. Kila kiungo katika mnyororo kinaweza kusababisha tukio la kuzama, au kupelekea kwenye kiungo chengine. Kujifunza kuogelea ni stadi ya msingi ya kuzuia kuzama, lakini ni muhimu pia ujumbe husika wa usalama ufundushwe ili watu wafahamu hatari zinazotokana na kuwa ndani au pembezoni mwa maji.



	Kutokujua hatari husika	Kukosekana kizuizi kwenye hatari	Kukosekana usimamizi wa kutosha	Kukosa uwezo wa kujikoa, au kuokolewa
Sababu	Ukosefu wa elimu ya usalama wa majini au hatari za mazingiri yanayokuzunguka.	Kuruhusu watu katika maeneo hatari ya maji - kama vile maeneo yenye mikondo ya nguvu.	Kuogelea sehemu zisizokuwa na mtu wa kukuoka.	Kutokuweza kuogelea mpaka kwenye usalama.
Jukumu la Mradi wa Usalama Majini	Kutoa elimu ya usalama wa maji kwa watumiaji .  Kupitia elimu hupatikana utambuzi na kwa utambuzi unaweza kujiepusha na hatari.	Kuwafahamisha watu maeneo salama ya kuingia majini.	Kuhamasisha watu kuwacha tabia ya kuingia majini peke yao, na kutoa usimamizi wa karibu kwa watoto wadogo	Kufundisha jamii kuogolea na uwokozi wa majini.

Viingo vitatu vya kwanza katika mnyororo wa kuzama vinaweza kupambanwa kwa ujumbe rahisi wa usalama majini. Aidha, baadhi ya mashirika na watu binafsi wanaweza kuwa na muda na nyenzo za kufundisha kuogelea na hivyo kukabiliana na kiungo cha mwisho katika mlolongo.

Mradi wa Usalama Majini umegawanyika katika sehemu mbili, ili kuruhusu mashirika kuchagua na kurekebisha sehemu ya mradi kulingana na mazingira na nyenzo zao.

## Kujua tatizo

Kwa nini na jinsi gani watu wanazama inasababishwa na vipi wamezungukwa na maji, uthubutu wao wanapokuwa ndani na pembezoni mwa maji, na uwezo wao wa kujiokoa. Kwa sababu hizi, kuzama huwaathiri makundi tofauti ya watu kulingana na mazingira wanayoishi na shughuli zao za kila siku.

Licha ya tofauti hizi, njia ya msingi ya kuzuia kuzama - kufahamu hatari na kuwa na uwezo wa kuogelea - ni mambo muhimu katika kuvunja mnyororo wa kuzama.

Unapoendesha mradi huu ni muhimu kuhakikisha kuwa wahusika sahihi wanalengwa. Hii itahakikisha kuwa mradi wako unalinda matukio mengi ya kuzama kwa gharama ndogo.

Unapoandaa mradi, ni muhimu kwa shirika kutambua ni nani wanalengwa na kwa namna gani. Hii itategemea kwa kiasi kikubwa juu ya nyenzo na wakati, na kama matokeo ya kuzama yanatokezea kwa kundi maalum la watu au kwa jamii nzima.

## Ambao wanaweza kuzama

Kuzama ni hatari kwa mtu yeote ambaye hufanya shughuli zake ndani au pembezoni mwa maji, bila ya kujali uwezo wake wa kuogelea - hata waogegeaji mahiri wanaweza kuzama.

Hatari ya kuzama inahusishwa sana na kuzungukwa na maji na uwezo wa kuogelea. Utafiti wa karibuni umeonyesha kwamba watu ambao hawajui kuogelea wako katika hatari zaidi ya kuzama.

Makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuzama kwa kawaida hujumuisha watu waliozungukwa na maji na hawajui kuogelea, au wasafiri ambao hutumia boti zisizo imara.

Watu katika makundi haya hutofautiana kulingana na mazingira yaliyowazunguka na sababu za kijamii. Kwa mfano, katika baadhi ya jamii inaweza kuwa wanawake ndio wanaopanda boti kufanya biashara sokoni, wakati katika jamii nyingine inaweza kuwa wanaume ndio hutumia boti kuendea kazini.

Kufahamu nani awe mlengwa, ni muhimu kushirikisha viongozi wa jamii na wanajamii kuwatambua watumiaji wa maji wa mara kwa mara. Hata hivyo, kwa ujumla unaweza kuwaweka katika makundi matano makuu:

1. Watoto wenye umri wa chini ya miaka 5
2. Watoto wenye umri wa miaka 5–14
3. Vijana na watu wazima wa kike
4. Wavuvi
5. Wasafiri.

# Kufahamu mchakato wa kuzama

## Makundi yaliyo hatarini

### 1. Watoto wenge umri wa chini ya miaka 5

Watoto wenge umri wa chini ya miaka 5 wako katika hatari kubwa ya kuzama kama wataachwa bila ya usimamizi wa kutosha.

Watoto wenge umri huu mara nyingi hutangatanga mbali na udhibiti wa wazazi wao na wako katika hatari ya kuanguka kwenye maji yasio na uangalizi.

Kufa kwa kuzama katika umri huu mara nyingi hutokezea wakati wazazi wameshughulika na kazi za nyumbani, kama kupika na kusafisha.

Ni vigumu kumfundisha mtoto wa chini ya miaka 5 kuogelea. Ujumbe wa usalama majini na ujuzi wa kuokoa unaweza kufundishwa kwa wazazi na wasimamizi.



### 2. Watoto wenge umri wa miaka 5–14

Katika umri huu watoto huanza kuoga peke yao na pia hufurahia kucheza majini na rafiki zao. Katika jamii nyingi shughuli za kuoga hufanyika katika maeneo yaliojitenga, mbali na usimamizi wa watu wazima.



### 3. Vijana na watu wazima wa kike

Kama vile shughuli za kila siku za kuoga, katika tamaduni nyingi vijana na watu wazima wa kike hutumia vyanzo vya maji kufanya kazi za nyumbani kama vile kufua nguo, kuteka maji au kuosha vyombo.

Ingawa shughuli hizi kikawaida hufanyika katika maji ya kina kifupi, kuingia katika maji ya kina kirefu kwa bahati mbaya au mkondo mkali wa maji huweza kusababisha kuzama. Aidha, mara nyingi wanawake huingia majini wakiwa wamevaa mavazi ya kikamilifu, na hivyo kufanya kuwa vigumu zaidi kueleha hata kama wanajua kuogelea.





## 4. Wavuvi

Wavuvi wako katika hatari ya kuanguka majini na pia wanakabiliwa na hatari zaidi kwa kuwa mbali na usalama na katika maji mabaya. Pamoja na kuwa majini kila siku, wavuvi wengi hawawezi kuogelea na hawapendelei kucaa makoti la kuokolea maisha.

## 5. Wasafiri

Kwa jamii za visiwani na ziishio karibu na mito, usafiri wa boti ni muhimu kwa biashara. Boti hizi mara nyingi hujazwa kupita kiasi, hukosa uangalizi mzuri na huwa na ukosefu wa vifaa vya kuokolea maisha kama boti za hakiba na makoti ya kuokelea maisha.

Majanga ya boti hutokea mara kwa mara Afrika. Abiria wa boti wafundishwe jinsi ya kutumia vifaa vya kuokolea maisha ili kuokoa maisha yao pindipo meli ikizama au wakianguka majini.

Ni muhimu kwa waendeshaji wa boti kufahamu wajibu wao wa kuwaweka watumiaji wake salama. Pindipo abiria watafahamu umuhimu wa vifaa vya kuokolea maisha, itawalazimisha waendeshaji kuweka vifaa hivyo botini.



# Mradi wa Usalama Majini

## Nini jukumu la Mradi wa Usalama Majini?

Ni jukumu la Mradi wa Usalama Majini kuzuia kuzama kwa:

- kutoa ujumbe wa usalama majini
- kuwafundisha watu jinsi ya kujiokoa wenyewe majini
- kuwafundisha watu jinsi ya kuwaokoa wengine majini.

### Sehemu ya 1: Elimu kwa Jamii – Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini

Vifo vingi vya kuzama vinaweza kuepushwa kwa kujifunza  
vipi kujiweka salama ndani na pembezoni mwa maji, na vipi  
kuwaweka wengine salama.

Sehemu ya Elimu kwa Jamii ina mambo 10 ya ujuzi wa usalama  
wa majini ambayo ni muhimu, rahisi na huweza kufundishwa  
bila ya haja ya kuingia majini.

Sehemu hii inaweza kufundishwa peke yake, au kama sehemu  
ya mafunzo ya Kujiokoa na Kuokoa.



### Sehemu ya 2: Kujiokoa na Kuokoa

Vifo vingi vya kuzama hutokea wakati watu wasiojua  
kuogelea vizuri wanapoingia kwa bahati mbaya kwenye maji  
mengi wasiyoweza kusimama. Sehemu hii inafundisha jinsi  
ya kujiokoa na huropa washiriki ujuzi wa kuogelea au kuele  
majini na kusubiri msaada ufike.

Kuingia majini ili kuokoa watu wengine inaweza kuwa hatari  
kubwa. Watu wengi huzama wakijaribu kuwaokoa watu  
wengine. Washiriki wa sehemu ya Uokozi watafundishwa jinsi  
ya kuokoa watu kwa usalama bila ya kuingia majini.



Sehemu ya Kujiokoa na Kuokoa inahitaji eneo lenye maji  
safi na salama na yanayofaa kufundishia kuogelea. Kwa  
kupunguza hatari, washiri wote wawe na uelewa mzuri wa usalma wa majini.

## Njia za Kupeleka Ujumbe

Njia mbili za kupeleka ujumbe zinaweza kutumika kwenye Mradi wa Usalama Majini:

### 1. Ujumbe kwa Jamii

Ujumbe wa usalama majini ambao unaweza kufikishwa kwa kundi kubwa la watu kwa urahisi na haraka hutarishwa.

Mafunzo yanaweza kutolewa mashulenzi, mikutano ya vijiji au vikundi vya jamii. Aidha, ujumbe unaweza kutangazwa magazetini, kwenye televisheni au redio.

Ujumbe unaweza kufundishwa kwa muda mfupi kwa gharama nafuu, na hauhitaji eneo la kuogelea.

### 2. Ujumbe kwa Walengwa

Kama kuzama kunajuulikana ni tatizo kwa sekta fulani ya jamii, basi mradi wa kina kwa walengwa unaweza ukaleta mafanikio makubwa kwa gharama ndogo.

## Fedha

Fedha zinahitajika kulipia vifaa na wafanyakazi. Fedha zinaweza kupatikana kwa:

### Ada ya Mafunzo

Katika baadhi ya maeneo watu wanaopata mafunzo wanaweza kuwa na uwezo wa kulipa kwa shirika linalotoa mafunzo. Wakati mwengine ada inaweza kulipwa na ushirika (kwa mfano shule au kundi la skauti), au na watu wenye wanaopokea mafunzo.

Kwa bahati mbaya, wale walio katika hatari kubwa ya kuzama hutokea katika koo maskini. Wanaweza kuwa hawana uwezo wa kulipa ada. Kama ada ya mafunzo inalipishwa, ni muhimu kuhakikisha kuwa maskini hawatengwi na mradi huu.

### Ruzuku

Fedha inaweza kupatikana kutoka kwa mashirika yanayotoa ruzuku au serekali. Ruzuku kwa kawaida hutolewa kwa lengo maalum. Ingawa lengo la msingi la Mradi wa Usalama Majini ni kulishughulikia suala la kuzama kama suala la afya, inawezekana pia kuomba fedha kuititia masuala ya kijamii, kama vile uongozi wa jamii, na michezo.

### Michango ya jamii

Kufa maji hugusa jamii nzima. Watu binafsi, mashirika na wafanyakabiashara lazima washajihishwe kusaidia utekelezaji wa Mradi wa Usalama Majini. Msaada unaweza kutolewa kwa njia mbalimbali - unaweza kuwa mchango wa kifedha au rasilimali.

# Sehemu ya 1: Elemu kwa Jamii – Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini



## Lengo

Lengo la Sehemu ya 1 ni kuwapatia wanafunzi elemu wanayoihitaji ili kuwa salama kwenye na karibu na maji.

Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini uliomo ndani ya sehemu hii umetaarishwa kwa kuzingizingatia urahisi wake wa kufahamika ili uweze kufikishwa kwa makundi makubwa kwa haraka na urahisi.



Matokeo ya mafunzo:

1. Kufahamu kwa nini uendeshe Mradi wa Elimu kwa Jamii.
2. Kufahamu umuhimu wa mukutano wa wadau.
3. Kuwa na ufahamu wa mahitaji yanayohitajika.

### Kwa nini uendeshe Mradi wa Elimu kwa Jamii?

Kuzama ni katika sababu zinaongoza kusababisha vifo.

Mara nyingi kuzama kunaweza kuepushwa kwa kuchukua tahadhari ndogo tu. Ujumbe wa Usalama Majini umetengenezwa kuelimisha watu jinsi ya kukaa salama ndani na pembezoni mwa maji.

Ujumbe unaweza kufundishwa kwa kutumia nyenzo chache na katika maeneo ambayo si rahisi kujifunza kuogelea kutokana na magonjwa yatokanayo na maji au ukosefu wa eneo zuri la kujifunza kuogelea.

### Wasikilizaji

Ujumbe wa usalama majini umeandaliwa kuwa rahisi kuufikisha kwa watu wa rika zote. Unatakiwa umfae mtu ye yeyote anaeishi au kufanya kazi majini au pembezoni mwake. Ujumbe utaambatanishwa na picha na unaweza kutolewa kwa urahisi kwa makundi madogo au makubwa. Ujumbe unaweza kubadilishwa kulingana na mazingira husika.

# 1.1 Mipango na maandalizi

## Ufikishaji

Ujumbe wa usalama majini unaweza kufundishwa kwa makundi makubwa au madogo ya watu. Unaweza kufundishwa kwa muda mfupi kwa kutumia nyenzo chache sana na hazihitajii eneo la kuogelea.

Mafunzo yanaweza kutolewa shulen, mikutano ya kijiji au vikundi vya jamii. Aidha, ujumbe unaweza kutangazwa magazetini, kwenye televisheni au radio.

Njia rahisi ya kuwafikia idadi kumbwa ya watu ni kwa kutumia mitandao na miundombinu iliyopo.

Mafunzo ya kuwasilisha ujumbe yanaweza kutolewa kwa watu ambao tayari wana muingiliano na walengwa wako.

Watu hawa ni pamoja na:

- walimu wa skuli
- wafanyakazi wa kijamii
- viongozi wa skauti
- wazee wa jamii.



## Mkutano wa wadau

Kabla ya kuanza mradi wako, itisha mkutano wa wadau.

Wadau ni watu walio na uelewa wa tatizo au wana uwezo wa kusaidia utekelezaji wa mradi. Taarisha orodha ya wadau wote na uwaalike katika warsha ya kujadili malengo yako.

Mikutano ya wadau husaidia:

- kutambua matatizo kabla ya kuanza
- kujuu nani anaweza kusaidia mradi
- kuhakikisha kila mtu anajua na anaelewa nia yako.

Mikutano wa wadau pia ni njia nzuri ya kueneza ufahamu wa mradi, na kushirikisha watu katika kuzuia kuzama.

Daima wajuulishe wadau jinsi mradi unavyoendelea. Hii inaweza kufanikishwa kwa kupitia barua pepe au tovuti.



### Zana

Ujumbe wa usalama majini umeandalowi ili uweze kufundishika kwa zana chache tu. Sehemu hii haihitaji eneo la kuogelea.

Mambo pekee unayohitaji ni:

- zana za kufundishia zilizomo katika mwongozo huu
- watu wa kufundishwa
- walimu
- eneo linalokidhi haja.



### Walimu

Kumtambua mwalimu anayefaa kuelimisha jamii ni muhimu kwa mafanikio ya mradi. Walimu wazuri husababisha matokeo bora ya mafunzo – wanafunzi wanaweza kujifunza haraka na elimu hubaki nao kwa muda mrefu zaidi.

Walimu lazima wawe na shauku ya kuokoa maisha na nia ya kutoa elimu waliyonayo kuhusiana na usalama wa majini.

Hakuna mapendekezo ya kiwango cha chini cha umri kwa mwalimu wa Elimu ya Jamii.

Hata hivyo, walimu wote wanapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

- **Kuaminika** – kuaminiwa kupanga masomo ipasavyo.
- **Kutegemewa** – hufika masomoni kwa wakati.
- **Motisha** – huto mafunzo kwa kadri ya uwezo wao.
- **Kufahamu hatari za maji** – kuwa na uwezo wa kuboresha mradi kulingana na mazingira.

Walimu wote wapya wapewe ushauri sahihi ili waweze kuelewa kila ujumbe wa usalama majini.

## 1.1 Mipango na maandalizi

### Eneo

Karibu maeneo yote yanaweza kutumika kufundisha usalama wa majini, ilimradi wanafunzi wawe wanaweza kumsikia na kumuona mwalimu.

Ujumbe unaweza kufundishwa:

Darasani



Katika ukumbi wa jamii



Pwani





Matokeo ya kujifunza:

1. Kujua ujumbe wa usalama majini na jinsi ya kuufundisha.
2. Kufahamu mpangilio wa masomo.

### Ujumbe wa usalama majini

kuna ujumbe 10 ya usalama majini, iliyogawanyika katika mandhari tatu.

#### Mandhari ya 1: Itambue hatari

Ujumbe huu hufundisha jinsi ya kutambua hatari majini:

1. Jua hali ya maji na hali ya hewa kabla ya kuingia majini.
2. Pima kina cha maji na hatari zilizopo chini ya maji kabla ya kuingia majini.
3. Tambua uwepo wa wanyama.

#### Mandhari ya 2: Jiweke salama

Ujumbe huu hufundisha jinsi ya kujiweka salama ndani na pembezoni mwa maji:

4. Kamwe usiingie majini peke yako.
5. Tii alama za usalama na bendera za onyo.
6. Tambua jinsi gani na wakati gani wa kutumia koti la kuokolea maisha.
7. Daima mwambie mtu lini na wapi unapokwenda pembezoni mwa maji.


#### Mandhari ya 3: Waweke wengine salama

Ujumbe huu hufundisha jinsi ya kuweka watoto wengine salama ndani au pembezoni mwa maji:

8. Jifunze njia salama ya kuwasaidia wengine bila ya kujiweka wewe hatarini.
9. Daima simamia watoto ndani au pembezoni mwa maji.
10. Weka nyumba yako salama.

## 1.2 Kufundisha ujumbe

Kila moja kati ya ujumbe 10 ya usalama majini inaambatanishwa na:



Picha inayooeleza ujumbe

Maelezo ya kwanini ujumbe huu ni muhimu

Angalau kitendo kimoja cha kufanya mwanafunzi.

Angalau alama moja kwa ajili ya mwalimu kujihusisha na wanafunzi.

### Jinsi ya kufundisha ujumbe

Ujumbe unaweza kufundishwa kwa kutumia njia yoyote inayowafaa wanafunzi na mazingira. Wanawezwa kufundishiwa mitaala zilizopo au kama sehemu ya somo tofauti.

Mfano rahisi wa mpango wa somo umejumuishwa katika muongozo huu ili kusaidia walimu wapya katika kufundisha ujumbe. Somo hufuata mpangilio rahisi:

- Fundisha kila ujumbe kwa kuwashirikisha wanafunzi kwa kutumia vielelezo na mafunzo ya papo kwa papo.
- Watie moyo wanafunzi kukumbuka ujumbe kwa kutumia mazoezi ya ubunifu kama vile bango, wimbo au mchezo wa kuigiza.

Kama somo linafundishwa kama somo moja, mchakato huu uchukue takriban muda wa saa 1

### 1.3 Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini – Mpangilio wa somo

Malengo

Baada ya somo hili wanafunzi wanatakiwa kuweza:

- kutambua kila kadi ina maana gani kutumia elimu hii ili kuwasaidia kuwa salama ndani na pembezoni mwa maji.

Nyenko

- Kadi (x10).
- Eneo linaloofaa kufundishia.
- Karatasi na kalamu (sio muhimu).

Muda

Saa 1  
↑

1. Utangulizi

- Waambie wanafunzi jina lako (na waambie jina la shirika lako kama hawaliuju).
- Eleza kwamba watasoma kwa furaha jinsi ya kuwa salama ndani na pembezoni mwa maji.

Muda

Dakika 5  
↓

2. Zoezi la kujichangamsha

- Waeleze wanafunzi kwamba sisi tunatumia maji kwa shughuli nydingi tofauti. Wape wanafunzi mifano.
- Waombe wanafunzi wazungunze na jirani yao kwa dakika tano juu ya matumizi yao ya maji.
- Pita katika makundi yote na uyaulize jinsi yanavyotumia maji.
- Eleza jinsi maji yanavyoweza kuwa hatari sana pindipo ukiangulka majini au hali yake ikibadilika wakati umo ndani.

Muda

Dakika 5  
↓

# Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini - Mpangilio wa somo

## 3. Kadi

Tumia kadi (zinazofuata ukurasa ujao) kueleza kwamba kuna mambo ya rahisi unayowenza kufanya kuijweka wewe salama ndani na pembezoni mwa maji, na kuwaweka watu wengine salama nolani na pembezoni mwa maji.

Kila kadi ina ujumbe muhimu wa usalama majini, maelezo ya ujumbe huo, hatua na maswali ya kufundishia. Zimegawanywa katika mandhari tatu:

1. Itambue hatari.
2. Jiwewe salama.
3. Waweke wengine salama.

Kwa kila kadi:

1. Itambulishemandhari.
2. Onyesha picha ya kila kadi kwa kila kundi.
3. Soma ujumbe muhimu wa usalama majini.
4. Soma maelezo kwa nini ujumbe huo ni ujumbe muhimu wa usalama majini.
5. Elezea hatua za wanafunzi kuchukua nyumbani.
6. Kama inafaa, tumia masuali ya kufundishia kushirikiana na makundi.

## Muda



Dakika 25

## Maelezo

Inapowezekana, shirikisha darasa kwa kutumia vitu husika kama magongo marefu na makoti ya kuokelea maisha

## 4. Zoezi la ubunifu

1. Ligawe darasa katika makundi madogo.
2. Lipe kila kundi ujumbe mmoja wa kuzingatia.
3. Waambie wanafunzi watunge wimbo, mchezo wa kuigiza, hadithi au bango la ujumbe wa usalama majini.
4. Watake kila kundi kuwaonyesha kazi zao kwa wanafunzi wengine.

## Muda

Dakika 25


Mandhari: Itambue hatari

Kwa nini?

Jifunze jinsi ya kutambua hatari kwenye maji.

## Itambue hatari:

1. Ijue hali ya maji na hali ya hewa kabra ya kuingia majini



## Itambue hatari:

1. Ijue hali ya maji na hali ya hewa kabra ya kuingia majini

Kwa nini?

Hali ya maji inaweza kubadilika kwa haraka sana.

Hatua


- Daima muulize mwenyeji kama hali ya maji na hali ya hewa zinaruhusu kuingia majini.
- Kuwa makini na mabadiliko ukiwa majini.
- Usiingie majini kama chanzo cha maji kinefurika, au unaposikia radi na kuona umwesa.
- Usiingie majini kama kuna mkondo mkali.

Swali la kufundishia

Waulize wanafunzi nani wangelimuuliza kuhusu hali ya maji na hali ya hewa.

## Itambue hatari:

2. Pima kina cha maji na hatari zilokuwepo chini ya maji kabra ya kuingia majini



## Itambue hatari:

2. Pima kina cha maji na hatari zilizokuwepo chini ya maji kabla ya kuingia majini

kwa nini?

Kama huwezi kuona chini, ni vigumu kujua kama kuna hatari yoyote chini ya maji.

Unaweza kuingia katika kina kilichokuzidi kimo, au kujumiza na vitu vya hatari kama vige viliyovuyunjika au jiwe lenye makali. Unaweza hata kuzongwa na majani.

Hatua


- Muulize mwenyeji kuhusu kina cha maji na kama kuna shimo au mabadiiko ya ghafla ya kina.
- Inapowezekana, ingia majini polepole na tumia fimbo kupima kina cha maji ya mbele yako na hisi vitu viliyyopo chini ya maji.

Swali la kufundishia

Waulize wanafunzi aina gani ya hatari wanaweza kuzikuta chini ya maji.

# Itambue hatari:

3. Tambua uwepo wa wanyama



## **Itambue hatari:**

### **3. Tambua uwepo wa wanyama**

**Kwa nini?**

Baadhi ya maeneo yenye maji yana wanyama ambaao wanaweza **kuwa hatari kwa binaadamu.**  
**Wanaweza kukutafuna au kukuchoma unapowakaribia.**

**Hatua**

- Muulize mwenyeji kama kuna wanayama wowote wa hatari majini.
- Kuwa macho na angalia uwepo wa wanyama majini.
- Uki muona mnyama hatari toka nje ya maji mara moja.

**Swala la kufundishia**

**Waulize wanafunzi wanyama gani wanaweza kuwakuta majini.**



## Mandhari: Jiweke salama

Kwa nini?

Jifunze jinsi ya kujiweka salama ulkiwa  
ndani au pembezoni mwa maji.

## Jiweke salama:

### 4. Usiingie majini peke yako



## Jiweke salama:

### 4. Usiingie majini peke yako

Kwa nini?

Ukiingia majini na wenzio, wanaweza kuwa na uwezo wa kukusaidia ukipatwa na matatizo au wanaweza kukutafutia msaada.

Hatua


- Daima ingia majini na rafiki yako au mtu mzima anaejua kuogelea.

Sualia la kufundishia

Waallize wanafunzi nani ambaye wangeweza kwenda nae majini.

## Jiweke salama:

5. Tii alama zote za usalama na bendera za onyo



## Jiweke salama:

5. Tii alama zote za usalama na bendera za onyo

Kwa nini?

Baadhi ya maeneo ya maji yana alama au bendera za kukuonya kama ni hatari kuingia majini.  
Kunaweza kuwa na vitu vya hatari chini ya maji au mkondo mkali.

Hatua


- Daima muulize mwényeji maana ya alama au bendera, na utii onyo lake.

Swali la somo

Waulize wanafunzi kama kuna alama yoyote ya onyo au bendera pembezoni mwa maji.  
Zinamaanisha nini?

## Jiweke salama:

6. Tambua jinsi gani na wakati gani wa kutumia koti la kuokolea maisha



## Jiweke salama:

6. Tambua jinsi gani na wakati gani wa kutumia koti la kuokolea maisha

Kwa nini?

Koti la kuokoa maisha hukuvezesha kuelea pindipo utaanguka majini. Yanakuwa na rangi za kungara na huwa na firimbi unayoweza kuiliza ili kuwaita waokowaji.

Huhakikisha huzami pindipo umeumia, umechoka au umezimia.

Hatua

- Kabla ya kusafiri na boti hakikisha makoti ya kuokolea maisha yanapatikana humo.
- Katika hali ya dharura, vaa koti la kuokolea maisha na ulifunge barabara.
- Kama hakuna makoti ya kuokolea maisha ya kutosha, shikilia vitu vinyavyoolea.


Kama inawezekana onyesha darasani jinsi ya kuwaa koti la kuokolea maisha.

Masuali ya kufundishia

Waulize wanafunzi kama washawahi kuvaa au kuona koti la kuokolea maisha. Wapi wameliona?

Waulize wanafunzi kitu gani kinachoelea watashikilia kama kutakuwa hakuna makoti ya kutosha

**JiWeke salama:**  
7. Daima mwambie mtu wapi na wakati gani unakwenda pembezoni mwa maji



## Jiweke salama:

7. Daima mwambie mtu wapi na walkati gani unakwenda pembezonii mwaa maji

kwa nini?

Utapokutwa na matatizo kuna mtu atajua sehemu ulipo, na wanawenza kuja kukusaidia.

Hatua

- Hakikisha unamwambia mtu wapi unakwenda, saa ngapi utarudi na njia gani utapita wakati wa kwenda na kurudi ili wajue wapi wanawenza kukupata.

Suala la kufundishia

Waullize wanafunzi nani watamuambia wanapokwenda majini au pembezonii mwake.



Mandhari: Waweke wengine salama

Kwa nini?

Jifunze jinsi ya kuwaweka wengine salama  
ndani au pembezoni mwa maji.

**Waweke wengine salama:**  
8. Jifunze njia salama za kuwasidia wengine bila za kuijweka wewe hatarini



## Waweke wengine salama:

8. Jifunze njia salmaa ya kuwasaidia wengine bila ya kijiweka wewe hatarini

### Kwa nini?

Kuokoa mtu majini kwa kuogelea inaweza kuwa hatari sana.  
Watu wengi huzama wakati wakijaribu kuwaokoa watu wengine.

### Hatua


- Ukiimuona mtu anataka kuzama, tumia kitu kirefu kama gongo kuwafiki, au warushie kitu kinachoelea kama geloni tupu.
- Kama hukupata gongo wala kitu kinachoelea, nenda ukatafute msaada.

### Swala la kufundishia

Waulize wanafunzi kitu gani kinachoelea wangeweza kutumia kumrushia mtu ili kimsaidie kumuoko.

## Waweke wengine salama:

9. Daima simamia watoto waliopo ndani au pembezoni mwa maji



## **Waweke wengine salama:**

**9. Daima simamia watoto walliyo ndani au pembezoni nwa maji**

**Kwa nini?**

Mtoto anaweza kuenda mbali na wewe na kuanguka majini.

**Hatua**


- Kamwe usimuache mtoto peke yake anapokuwa ndani au pembezoni mwa maji.
- Kama inakubidi ufanye shughuli nyengine wakati huo huo, muombe mtu mwingine awesimamie watoto.

**Suala la kufundishia**

*Waulize wanafunzi vitu gani vinavyowenza kuwashughulisha wanaposimamia watoto.*

## Waweke wengine salama:

10. Weka nyumba yako salama



## **Waweke wengine salama:**

### **10. Weka nyumba yako salama**

**Kwa nini?**

*Watoto wanaweza kuanguka kwenye maji yasiyokuwa na uzio ndani au karibu na nyumbani.*


**Hatua**

- Kumbuka kufunika ndoo, vyoo na mapipa ya kuhifadhi maji.
- Daima funga milango na kuzuwa watoto wadogo kuzurura një peke yao.

**Masuali ya kufundishia**

*Waulize wanafunzi aina gani ya maji yaliotuwama wanayo ndani na pembezoni mwa nyumba.  
Wanaweza kufanya nini kuyalinda?*

# Sambaza ujumbe!



## Sehemu ya 2: Kujiokoa na Uokoaji



### Lengo

Lengo la Sehemu ya 2 ni kuwapatia wanafunzi ujuzi wa vitendo wanaouhitaji kujiokoa wenyewe kama watapata matatizo majini, na kuwaokoa wengine.

## 2.1 Mipango na maandalizi



Matokeo ya kujifunza:

1. Kufahamu muda gani unahitajika kuendesha sehemu hii.
2. Kufahamu ujuzi na sifa zinazohitajika kuwa mwalimu.
3. Kufahamu jinsi ya kutambua eneo salama la kufundishia.
4. Kufahamu jinsi ya kukagua eneo la kufundishia kama lina hatari.
5. Kufahamu jinsi ya kulitaarisha eneo la kufundishia.
6. Kufahamu viafaa gani vinahitajika kuendesha sehemu hii.

### Vitendea Kazi

Kutoa mafunzo ya Kujiokoa na Uokoaji unahitaji:

- zana za kufundishia zilizopendekezwa na muongozo huu
- wanafunzi wa kufundisha
- muda wa kutoa masomo yote
- walimu wenye uwezo
- sehemu inayofaa kuogelea
- vifaa vya kufundishia.

### Muda

Urefu wa muda utaowachukua wanafunzi kujifunza ujuzi wote wa sehemu ya Kujiokoa na Uokoaji utatofautiana kulingana na mambo mengi. Hata hivyo, wanafunzi wengi watakuwa na uwezo wa kukamilisha sehemu hii kwa kipindi cha masaa 15–20.

Kuwapeleka wanafunzi kwenye eneo linalofaa kufundishia inaweza kuwa vigumu kwa hiyo sehemu hii imegawanywa katika masomo 13, kila moja ikiwa na matokeo maalum.

Kila somo limebuniwa kufundishwa kwa wastani wa dakika 90. Inapendekezwa kwamba, kuwe na muda wa mapumziko angalau mara moja katika kipindi hichi.

Wakati walimu na mashirika yatapokuwa mazoefu katika ufundishaji na usimamizi wa masomo wanaweza kurekebisha mipango ya somo ipasavyo.



### Walimu

Sehemu muhimu ya Kujiokoa na Uokoaji ni kwamba wanafunzi pia wana haja ya kufundishwa ujumbe muhimu wa usalama majini. Walimu kwa hiyo wanahitaji kuwa makini wanapofundisha Sehemu ya 1: Elimu kwa Jamii - Ujumbe Muhimu wa Usalama Majini.

Walimu wana wajibu kwa ustawi wa wanafunzi. Ni lazima wahakikishe usalama unakuwepo muda wote wa somo.

Mbali na ujuzi na sifa zilizopendekezwa kwa walimu wa Elimu kwa Jamii (ukurasa wa 15), inapendekezwa kuwa walimu wa Uokozi na kujiokoa wawe:

- angalau wana umri wa miaka 16
- wana mawasiliano mazuri na jamii
- waogeliaji wenye uwezo wakuogelea angalau mara mbili ya urefu wa eneo la kufundishia
- wenye uwezo wa kuokoa
- wenye uwezo wa kutoa huduma ya kwanza inapohitajika.

### Kuchagua sehemu salama ya kufundishia kuogelea

Aina ya maji yanayotumika kufundishia yatatofautiana kulingana na msimu na jiografia ya mahala hapo. Baadhi ya mashirika wanaweza kupata bwawa maalum la kuogelea, lakini wengi itawabidi kutumia mito, maziwa, mabwawa au bahari.

Kama maji yako katika eneo binafsi, ni muhimu kupata ruhusa kutoka kwa mmiliki kabla ya mafunzo kuanza.

## 2.1 Mipango na maandalizi

Ufaaji wa eneo utategemea jinsi gani eneo hilo ni salama. Usalama huo husababishwa na mambo kadhaa:

### Hali ya hewa na kupwa na kujaa

Kwa nini: Maji asili yanaweza kubadilika kulingana na hali ya hewa, na katika baadhi ya wakati kupwa na kujaa. Eneo linaweza kuwa salama wakati wa jua lakini hatari baada ya mvua.

Jinsi ya kulinda:

Muulize mwenyeji vipi hali ya maji inavyobadilika na hali ya hewa na kupwa na kujaa.



### Kasi ya maji

Kwa nini: Kama maji yana kasi kubwa, wanafunzi wanapata shida kufanya mazoezi, na walimu hawataweza kuangalia darasa kwa ufanisi.

Jinsi ya kulinda:

Jaribu kutafuta eneo ambalo kasi ya maji yake ni ndogo iwezekanavyo, inapendezwa iwe ni ndogo kuliko nusu ya kasi ya wanafunzi kutembea. Chunguza kwa kutupa kitu kinachoelea majini.



### Chujio

Kwa nini: Chujio ni kitu kinachoruhusu maji kupita chini yake. Chujio ni hatari sana kwa sababu linaweza kushikilia mtu chini ya maji. Mfano wa chujio pichani kulia, inaonyesha matawi ya mti ulioanguka.



Jinsi ya kulinda:

Masomo ya kuogelea na vitendo kamwe yasifundishwe kuelekea kwenye chujio.

### Kina cha maji

Kwa nini: Wanafunzi wanaweza kuanguka kwenye maji ya kina kirefu zaidi ya uwezo wao.

Jinsi ya kulinda:

Kina cha maji kinachofaa kufundishia kuogelea hutegemea kiwango cha wanafunzi. Wanaoanza wafundishwe kwenye maji ya kifua, lakini pale uwezo na kujiamini unapo ongezeka, kina cha maji kinaweza kuongezwa.



## 2.1 Mipango na maandalizi

### Mteremko


Kwa nini: Kama mteremko ni mkali wanafunzi wanaweza kuingia kwenye maji ya kina kirefu kwa bahati mbaya. Kwenye mteremko mkali ni vigumu pia kuongeza kina hatua kwa hatua ili kujenga kujiamini kwa wanafunzi.



Jinsi ya kulinda: Eneo la kufundishia lenye mteremko mdogo litumike. Tembea kwa makini kwenye eneo la kufundishia ili kuhakikisha kuwa hakuna mashimo au miteremko mikali ambayo wanafunzi wanaweza kuangukia.

### Vitu chini ya maji

Kwa nini: Wanafunzi wanaweza kujiuza kwenye kitu kikubwa au chenye ncha kali, au kujizonga na kamba au mimea. Vihatarishi vya kawaida ni pamoja na magugu, miamba mikubwa na vigae viliviyovyunjika.



Jinsi ya kulinda: Kwa uangalifu tembea kwenye eneo la kufundishia kuhakikisha hakuna vitu vya hatari chini ya maji.

### Wanyama wa hatari

Kwa nini: Wanyama wa hatari wanaweza kusababisha kuumia kwa manafunzi au mwalimu wakati wa somo. Wanyama hawa wanaweza kuwa majini au pembezoni mwake. Mifano ni pamoja na mamba, papa na mchwa.



Jinsi ya kulinda: Zungumza na wenyeji ili kujua kama kuna wanyama wowote wa hatari katika eneo hilo.

### Magonjwa yanayoanza majini

Kwa nini: Magonjwa mengi hupatikana kwa kutumia maji yenye vidudu vya maradhi hayo.

Jinsi ya kulinda: Epuka kufundisha kwenye maji yanayojuulikana kuwa na vidudu vya maradhi. Kama huna uhakika, wasiliana na mamlaka ya afya.

### Mazingira machafu

Kwa nini: Kuogelea kwenye maji machafu inaweza kusababisha maradhi makubwa.

Jinsi ya kulinda: Epuka kufundisha kwenye maji yaliyo karibu na bomba la maji machafu, viwanda au bandari. Kama huna uhakika, wasiliana na mamlaka ya afya.



## 2.1 Mipango na maandalizi


### Kukagua eneo la kufundishia

Njia rahisi ya kukagua hatari zilizopo chini ya maji ni kutembea taratibu na kwa makini kwenye eneo la kufundishia, huku ukihisi vitu vilokuwepo chini ya maji kwa kutumia fimbo.

Kamwe usikague eneo peke yako kwa kuzingatia unaweza kukutwa na matatizo.



Kuanzia kwenye kipembe, taratibu tembea kwa mfumo wa zigizaga kwenye eneo la kufundishia huku ukikagua chini ya maji kwa kutumia fimbo. Endelea na utaratibu huu mpaka utapohakikisha umekagua eneo lote.



Kama watu zaidi watapatikana, jipangeni bega kwa bega kwenye mstari ulonyooka pembezoni mwa eneo la kufundishia. Songeni mbele kwa pamoa, huku mkikagua vitu vilivyo chini ya maji mpaka mufike upande wa pili.



### Eneo la kuogelea – orodha ya ukaguzi

Tumia orodha ifuatayo kuchagua eneo linalofaa kufundishia kuogelea.

Kama jibu lako ni hapana kwa mojawapo wa maswali, basi eneo hilo halifai kufundishia na hivyo eneo jengine litafutwe.

Mbali na orodha, ushauri wa kina ni lazima upatikane kutoka kwa wenyeji ili kuhakikisha kwamba eneo hili halina hatari nyenginezo.

Mazingatio	Ndio	Hapana	Hajulikani
Je, kwa kawaida watu huingia majini?			Waulize wenyeji kwa ushari.
Je, kasi ya maji ni ndogo kuliyo nusu ya kasi ya kutembea kwa miguu?			angalia kwa kurusha fimbo majini.
Je, maji yanapotiririkia hakuna chujio?			Nenda yanapotiririkia maji na uangalie.
Je, eneo halina mabadiliko ya ghafla ya kina?			Kagua kwa kutembea kwenye eneo
Je, kuna mteremko mdogo?			Kagua kwa kutembea kwenye eneo
Je, eneo la kufundishia halina vitu vya hatari chini ya maji?			kagua kwa kutembea kwenye eneo
Je, eneo la kufundishia halina wanayama hatari?			waulize wenyeji kwa ushauri
Je, eneo halina wadudu wa maradhi?			waulize wenyeji au mamlaka ya afya
Je, eneo halina uchafu?			waulize wenyeji au mamlaka ya afya

## 2.1 Mipango na maandalizi

### Kutaarisha eneo la kufundishia

Baada ya kuchagua eneo salama la kufundishia kuogelea ni muhimu mipaka ya eneo hilo iwekwe wazi.

Eneo lilowekwa wazi mipaka yake:

- hupunguza uwezekano wa wanafunzi kutembea au kuogelea kwenye maji ya hatari
- inakuwezesha kuwaweka wanafunzi pamoja, na kufanya kuwa rahisi kuangalia wanafunzi wanapofanya mazoezi ya kuogelea
- inamuezesha mwalimu na wanafunzi kuona maendeleo kwa sababu wanaweza kuona umbali gani inawabidi waogelee.

Eneo la kufundishia liwe kubwa vya kutosha kuendeshea masomo kwa usalama. Wanafunzi wawe na nafasi ya kutosha kufanya mazoezi ya stadi zao, na mwalimu awe na uwezo wa kuwafikia wanafunzi haraka pindipo wakipata matatizo.

Kuliwekea mipaka utahitaji:




Kamba iliyokoza na inayoelea



Vitu vinavyoolea  
(kama mageloni matupu)



Vitu vinavyozama  
(kama mageloni yenye mchanga)



Kuliwekea mipaka eneo:

- Weka kitu kinachozama katika kila kipembe.
- Weka kitu kinachoelea katika kila kipembe na ukifunge na kitu kinachozama kwa kutumia kamba.
- Uganisha vitu vinavyoolea kwa kamba.
- Ongeza vitu vinavyoolea kwenye kamba ili ipate kuelea.

Kwenye maeneo yanayojaa maji, angalia kina cha maji kila baada ya dakika 10 na rekebisha eneo inapolazimika

### Vifaa vya kufundishia

Vifaa bora vya kufundishia vinasaidia sana katika kufundisha wanafunzi wapya.

#### Kitu kinachoelea

Kitu kinachoelea ni kifaa muhimu kinachoweza kutumika kutoa msaada kwa mwanafunzi wakati wakiongeza ujasiri wao kwenye maji.

Katika baadhi ya nchi, vifaa maalum vya kuelea vimetengenezwa kwa ajili ya kufundishia kuogelea. Hata hivyo, katika maeneo ambayo vifaa maalum havipatikani au ni ghali, vifaa mbadala vya kienyeji vinaweza kutumika.



Vifaa vya kuelea vinatakiwe viwe:

- Rahisi kukishikilia
- Rahisi kukitembeza majini
- Kina uwezo wa kumfanya mwanafunzi aelee majini.

Wanafunzi wote wanahitaji kifaa cha kuelea kwa kipindi chote cha sehemu ya Kujiokoa na Uokoaji.

Mifano ya vitu vya kuelea vinavyofaa ni pamoja na:

#### Boya la kuogelea

Boya la kuogelea limetengenezwa hasa kwa kufundishia kuogelea. Mara nyingi hutengenezwa ka fomu na yanapatikana katika maduka mengi ya michezo.

Yanaweza kuwa na umbo la mstatili, au marefu, duara na membamba (Ona kulia).



Faida:

Rahisi kushikilia.

Hasara:

Ghali na hayapatikani katika maeneo mengi.

#### Mageloni

Geloni tupu (angalau la lita 5) linaweza kushikilia uzito wa mtoto au mtu mzima kwa urahisi. Mageloni mengi yana mkono ambaao wanafunzi wanaweza kushikilia wakiwa majini. Chombo kinapaswa kusafishwa vizuri kabla ya kutumiwa.



Faida:

Rahisi na inapatikana katika maeneo mengi.

Hasara:

Sio rahisi kushikilia wakati ukiogelea.

## 2.2 Maandalizi ya somo



Matokeo ya kujifunza:

1. Kufahamu jinsi mwalimu anavyoweza kukaa salama.
2. Kufahamu jinsi ya kuwaweka wanafunzi salama.
3. Kufahamu jinsi ya kuandaa na kutaarisha darasa.

### Usalama wa mwalimu

Walimu wa kuogelea hutumia masaa mengi majini au pembezoni mwake na wanaweza kuwa hatarini. Hatari hizi zinaweza kupunguzwa kwa kuzitambua hatari zenyewe na kwa kuchukua tahadhari ndogo.


### Mavazi sahihi

Mavazi sahihi yanamruhusu mwalimu kuonekana na kutambulika na wanafunzi na walimu wengine kwa urahisi. Pia inamfanya mwalimu kuonekana mtaalamu.

Mavazi yanayotumika wakati wa kufundisha lazima yamkinge juu mwalimu na yawe rahisi kufanya kazi. Yawe yanamruhusu mwalimu kufanya wajibu wake, ikiwa ni pamoja na kuonyesha mfano majini au kumuokoa mwanafunzi aliepata matatizo.

Kuwa na nguo safi na zenyewe mvuto wa kitaalamu inaongeza mtazamo wa mamlaka ya mwalimu na inafanya iwe rahisi kwa mwalimu kuingiliana na wanafunzi na wazazi.


Walimu wafunike ngozi zao kwa kutumia nguo popote inapowezekana.



### Usalama juani

Jua hutoa mwanga duniani, na sehemu ya mwanga huo ni miale hatari. Miale hii inapopiga kwenye ngozi, husababisha kubadilika kwa rangi, kuungua na maharibiko mengine ya ngozi.

Kupigwa sana na jua kunaweza kusababisha saratani ya ngozi na maradhi ya macho. Bila ya kujilinda vya kutosha, walimu wako kwenye hatari ya kupigwa na jua kupita kiasi. Madhara ya jua yatategemea aina ya ngozi lakini walimu wanatakiwa wawe na ufahamu wa kinga zinazoweza kuchukuliwa ili kupunguza hatari:



#### Kivuli

Kila iwezekanapo jaribu kufundisha kivulini.

#### Mafuta ya jua

Katika baadhi ya nchi mafuta ya jua yanapatikana kupunguza makali ya miale hatari.

#### Jifunike

Wakati ukifundisha, kama inawezekana vaa fulana, kofia na miwani ya jua inayolinda macho na miale hatari.



#### Maji

Kunywa maji mara kwa mara ili kuepusha ukosefu wa maji mwilini.

## 2.2 Maandalizi ya somo



### Usalama wa wanafunzi

Ni jukumu la mwalimu kuwaweza wanafunzi salama kabla, wakati na baada ya somo. Ili kufanikisha haya mwalimu lazima:

- **awe na ufahamu mzuri wa mradi**  
Mwalimu awe na ufahamu mzuri wa maudhiui na ajue jinsi ya kuubadilisha kulin-gana na kiwango cha ujuzi wa wanafunzi.
- **awe na ufahamu mzuri wa mazingira ya kufundishia**  
Mwalimu awe anafahamu hatari za mazingira anayofundishia na awe na ufahamu wa mabadiliko ya hali ya maji na hali ya hewa.
- **awe na ujuzi wa kuokoa**  
Mwalimu lazima awe na uwezo wa kutoa msaada wa haraka kwa mwanafunzi mwenye matatizo majini au nchi kavu.
- **awe na uwezo wa kuandaa darasa**  
Mwalimu awe na uwezo wa kuandaa darasa ili kuhakikisha kwamba ukubwa wa darasa ni sahihi na wanafunzi wana uwezo sawa.
- **awe na uwezo wa kusimamia darasa**  
Darasa liwe chini ya udhibiti wa mwalimu wakati wote.

### Kufanya eneo la kufundishia kuwa salama

Eneo la kufundishia lazima lichunguzwe kabla ya kutumika (angalia ukurasa wa 52).

Wakati ukitumia eneo la kufundishia:

- Kusanya vifaa vyote kabla na baada ya kutumia – vifaa vilivyoachwa ovyo vinaweza kukukwaa.
- Angalia wanyama hatari.
- kuwa muangalifu na ukali wa jua – hakikisha wanafunzi hawapigwi na jua kwa muda mrefu bila ya kupata mapumziko. Tumia mwongozo wa usalama juani (ukurasa 57).
- Kuwa mwangalifu na mabadiliko ya hali ya hewa – Hali ya hewa inaweza kubalika haraka, na kushawishi mtiririko wa maji na mazingira ya kufundishia.

### Mavazi sahihi

Baadhi ya vitambaa vinanyonya maji mengi na vinaweza kuwa vizito pindi vikiroa. Ni vigumu kujifunza kuogelea katika mavazi yaloroa.

Hata hivyo, kutokana na sababu za kitamaduni na kidini, katika nchi nydingi ni muhimu kujistiri. Walimu wawahimiza wanafunzi kuvalaa nguo ambazo hazinyonyi maji mengi na hazizuwii matumizi ya mikono.



### Hali ya kiafya

Walimu wafahamu hali ya kiafya ya wanafunzi, na wafahamu jinsi hii inavyoweza kuathiri uwezo wao wa kufanya mazoezi majini.

Kama huna uhakika basi tafuta ushauri wa kiafya iwezekanapo.

Kwa ujumla, wanafunzi wenye hali zifuatazo watolewe kwenye masomo hadi hapo watakapo pona kikamilimu:

- vidonda vilivyo wazi
- mafua na kikohozi
- maradhi ya macho
- mashikio yalioathirika.

### Msaada

Walimu wote wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwasaidia wanafunzi wakipata matatizo wakati wa mafunzo. Wanafunzi wanaweza kuhitaji kuokolewa wakiwa katika shida au wakiwa wameumia.

## 2.2 Maandalizi ya somo

### Maandalizi ya darasa

#### Ukubwa wa darasa

Ni muhimu kuhakikisha kwamba ukubwa wa darasa ni unaofaa ili kuhakikisha kuwa:

- wanafunzi wanaweza kumuona na kumsikia mwalimu
- wanafunzi wanaweza kupiga hatua kwa kasi inayofaa
- wanafunzi wana nafasi ya kutosha ya kufanya mazoezi
- inawezekana kuhakikisha usalama wa wanafunzi.

Ukubwa wa darasa la kuogelea litategemea:

- **ngazi ya ujuzi ya wanafunzi**

Wanafunzi wapya wanahitaji kushughulikiwa zaidi na mwalimu.

- **uharaka wa kujifunza kwa wanafunzi**

Watu hujifunzi kwa kasi tofauti. Wanafunzi wanaojifunza polepole watahitaji kushughulikiwa zaidi na mwalimu.

- **uzoefu wa mwalimu**

Mwalimu mwenye uzoefu anaweza kuwa na uwezo wa kusimamia idadi kubwa ya wanafunzi.

- **ukubwa wa eneo la kufundishia**

Wanafunzi wanapaswa kuwa na nafasi ya kutosha kufanya mazoezi ya stadi zao walizojifunza wakati wa masomo kwa raha.

- **usalama wa mazingira**

Usalama wa wanafunzi ni kipengele muhimu kuliko vyote katika kuamua ukubwa wa darasa. Kwa wanafunzi kuwa salama wakati wa masomo mwalimu lazima awe na uwezo wa kuwasiliana na wanafunzi wote na kuwasaidia katika dharura.

Ingawa mashirika yataamua wenyewe idadi ya wanafunzi ambao mwalimu anaweza kufundisha, inapendekezwa kwamba:

- walimu wasiokuwa na uzuwefu wafundishe si zaidi ya wanafunzi 6 kwa wakati mmoja.
- walimu wazowefu wafundishe si zaidi ya wanafunzi 10 kwa wakati mmoja.

### Kuwagawa wanafunzi

Wanafunzi watapiga hatua kwa kasi tofauti kutokana na sababu mbalimbali. Hata hivyo, maendeleo mazuri hupatikana wakati wanafunzi wanapofanya mazoezi na wenzao wenye uwezo sawa.

Uwezo unaweza kutathminiwa kwa kuauliza wanafunzi umbali gani wanaweza kuogelea, au inaweza kutathminiwa kwa uhakika mwanzoni mwa mafunzo.

Mara baada ya wanafunzi kutathminiwa kuna njia mbili za kuwagawa wanafunzi:

### Kuwagawa kwa madarasa


Idadi kubwa ya wanafunzi inaweza kugaiwa katika madarasa tofauti kulingana na uwezo wao.



### Makundi ndani ya darasa

Idadi ndogo ya wanafunzi inaweza kugawanywa kulingana na uwezo katika darasa moja.

Mwalimu aweke malengo tofauti kwa uwezo tofauti, na kwa ajili ya usalama ahakikishe wanafunzi wenye uwezo wa chini wanakaa karibu na mwalimu.



## 2.2 Maandalizi ya somo

### Maandalizi na usalama orodha ya ukaguzi

Kuangalia usalama wa wanafunzi wakati wa somo, mara kwa mara tathmini orodha iliyopo hapo chini:

Mazingatio	Ndio	Hapana
Je, wanafunzi wana uwezo sawa?		
Je, ukubwa wa darasa ni unalingana na uwezo wa mwalimu?		
Je, mwalimu anaweza kuwaona wanafunzi wote?		
Je, mwalimu anaweza kuwasikia wanafunzi wote?		
Je, wanafunzi wanaweza kumuona mwalimu?		
Je, wanafunzi wanaweza kumsikia mwalimu?		
Je, mwalimu anaweza kuingiliana na wanafunzi wote?		
Je, mwalimu anaweza kuwafikia wanafunzi wote kwa chini ya sekunde 5 ?		
Je, sehemu ya kufundishia imekaguliwa na uwepo wa hatari?		
Je, sehemu ya kufundishia ni kubwa vya kutosha kulingana na idadi ya wanafunzi?		
Je, wanafunzi wamevaa nguo sahihi?		
Je, kuna mwanafunzi yoyote mwenye hali ya kiafya inayoweza kuathiri uwezo wake wa kuogelea?		

## 2.3 Usimamizi wa darasa



Mtokeo ya kujifunza:

1. Kufahamu jinsi ya kuanzisha tabia.
2. Kufahamu jinsi ya kuwapa wanafunzi motisha.
3. Kufahamu jinsi ya kusimamia darasa majini.
4. Kufahamu mbinu zinazotumika kutoa mifano mizuri.


Kufundisha ujuzi wa kujiokoa inaweza kuwa kazi inayokuhamasisha na kukuridhisha. Kama zilivyo kazi zote za kufundisha, kuifanya vizuri kunahitaji uvumilivu, mazoezi na shauku kubwa. Pia inahitaji wanafunzi kuelewa kinachotarajiwa kutoka kwao, na kitu gani watarajie kutoka kwa mwalimu.

### Kuweka sheria

Ni muhumu kwamba wanafunzi wote wanajali usalama wakati wa somo. Mwalimu lazima awe na udhibiti kamili wa wanafunzi darasani na awe na uwezo wa kuwatowa wanafunzi majini haraka wakati wa dharura. Wakati wa somo la kwanza weka kanuni za nidhamu na usalama. Rudia kanuni kabla ya kuanza kila somo:

#### kanuni za nidhamu

- Daima msikilize mwalimu – mwanafunzi afanye tu yale aloambiba afanye na mwalimu.
- Daima tembea katika eneo la kufundishia, usikimbie.
- Vua mapambo na zifunge nyuma nywele refu.
- Simama mbali na maji mpaka uambiwe ingia majini.



## 2.3 Usimamizi wa darasa

### Kukabiliana na wanafunzi wasumbufo

Kama mwanafunzi anavunja kanuni mara kwa mara, muondoe majini na umuweke sehemu salama mbali na maji. Mueleze kwa nini ameondolewa darasani na kuwa atawea kurudi darasani pale watapokubali kufuata kanuni. Kama mwanafunzi atakubali basi mrudishe darasani.

### Kuweka matarajio

#### Desturi

Wanafunzi watakuja darasani pindipo wakiwa na uhakika kuwa mwalimu atakuwepo. Endeleva utaratibu wa kawaida:

- Anza na maliza kwa wakati wa kawaida.
- Wajuulishe wanafunzi wapi wasubiri kabla na baada ya somo.



### Motisha

Wanafunzi wana uwezekano mkubwa wa kuja darasani na kupiga hatua kwenye ujuzi wanaojifunza kama watakuwa na motisha.

Motisha inaweza kupatikana kwa:

- kuweka malengo yatakayofikiwa kwa muda mfupi mwanzo wa somo
- kuweka malengo ya muda mrefu yatakayofikiwa mwisho wa mafunzo
- kuwapa maoni chanya pale wanafunzi wanapofanya vizuri
- kujenga ujuzi kwa hatua - songa mbele pale utapojuwa kwamba ujuzi uliopita umefahamika vizuri.



Malengo yawekwe kulingana na uwezo wa mwanafunzi. Kuwalazimisha wanafunzi kujaribu jambo ambalo hawezi kufanikiwa itamvunja moyo mwanafunzi na inaweza kuwa hatari.

Wasifu wanafunzi watapofanya vizuri!

### Kujiweka

Ni muhimu kwa mwalimu kukaa sehemu ambayo daima atawaona wanafunzi na atawea kuwasaidia kwa haraka ikitokea dharura majini.

Mwalimu kamwe asiwape mgongo wanafunzi, na asiwaruhusu wanafunzi kuingia au kutoka majini bila ya usimamizi.

Daima wanafunzi waogelee kuelekea maji yenye kina kidogo (kwa kawaida kuelekea ufukweni) au sambamba na ufukwe ili kuepusha watoto kuingia maji yenye kina kirefu.




### Mazoezi

Na makundi makubwa ya watoto inaweza kuwa vigumu kuchunguza uwezo wa wanafunzi, dumisha usimamizi wa kutosha na hakikisha kwamba wanafunzi wana nafasi ya kutosha ya kufanya mazoezi.

Kupunguza darasa katika vikundi vidogo vidogo, wapangishe mstari wanafunzi na umpe kila mwanafunzi namba 1 au 2, au jina la kundi.

Wanafunzi wanaweza kuanza mazoezi pale mwalimu anapotaja nambari ya mwanafunzi.

Wanafunzi wasiofanya mazoezi wasimame wima kwenye mstari huku vichwa vyao vikiwa juu ya maji na wakisubiri zamu yao.



### Mfumo wa wawili wawili

Mfumo wa wawili wawili ni pale muogeleaji mmoja anapopewa mwenza mwenye uwezo sawa. Kila mmoja ana jukumu la kumuangalia mwenziwe. Kama mwenziwe amepata matatizo anaweza kumjuulisha mwalimu.

Kwa watoto wakubwa, mfumo wa wawili wawili unaweza kutumika kusaidia mazoezi ya mbini za kuogelea. Mwenza mwenye uwezo sawa anaweza kumsaidia mwenziwe kwenye maji, chini ya usimamizi wa mwalimu. hii ina maanisha kuwa wanafunzi wengi zaidi wanaweza kufanya mazoezi kwa wakati mmoja.

Mfumo wa wawili wawili uelezwe mwanzo wa kila somo.


## 2.3 Usimamizi wa darasa

### Mifano


Wanafunzi wanajifunza vizuri na kwa haraka kwa kuiga. Kuonyesha mfano ni bora kuliko maneno elfu moja na ni njia bora ya kufikisha ujumbe kwa wanafunzi. Kama wanafunzi watakuona ukifanya kitu wataamini kuwa ni sahihi.

Wakati ukionyesha mfano unapaswa:

- ufanye mfano kuwa rahisi na onyesha tu hatua unayojaribu kuifafanua
- hakikisha wanafunzi wanaweza kuona mfano
- hakikisha wanafunzi hawako majini kama mfano unaonyeshewa majini



- hakikisha wanafunzi wote wanaweza kukuona na kukusikia kama mfano unafanywa nchi kavu
- fanya mfano katika mwelekeo ule ule unaotaka wanafunzi kuogelea.



## 2.4 Ujuzi wa uokuaji kwa walimu



Matokeo ya kujifunza:


1. Kujua jinsi ya kupata msaada.
2. Kufahamu jinsi ya kufanya uokozi wa nchi kavu.
3. Kufahamu jinsi ya kufanya uokozi wa kuogelea.

Ingawa maandalizi mazuri ya somo hupunguza ajali nyingi, haitozuwia ajali zote kutokea. Mwalimu wa kuogelea ajitaarishe kuchukua hatua za dharura kutoa mshaada kwa wanafunzi majini au nchi kavu.

### Kupata msaada

Ni muhimu kwa walimu wengine na wanafunzi kufahamu kwamba uwokoaji unafanyika. Wanaweza kutoa msaada kwenye uokozi au kwenda kuita msaada ulio mbali zaidi pindi ikihitajika.

Kuashiria kuwa unachukua hatua za dharura, piga kelele na puliza filimbi yako mara 3:



## 2.4 Ujuzi wa uokoaji kwa walimu

### Wapeleke wanafunzi eneo salama

Wakati wa uokoaji, wanafunzi wengine wanaweza kuwa bado wako majini. Ni muhimu kuhamia katika eneo salama.

Tumia sauti na ishara za mikono kuwahamasisha wanafunzi kuogelea kwenda pembezoni au eneo salama wanaweweza kusimama na kusubiri maelezo zaidi kutoka kwa mwalimu.



### Anzisha mawasiliano ya sauti

Wakati wa uokoaji ni muhimu kuanzisha na kudumisha mawasiliano ya sauti kumtuliza mwanafunzi na kumpa maelekezo ya jinsi gani wanaweza kujisaidia wenyewe.

Katika baadhi ya matukio, kutoa maelezo - kama vile "weka miguu yako chini na simama" - inaweza kuwa ni uwokozi tosha.



"Weka miguu yako chini."

"Weka kichwa chako juu ya maji"

"Tulia. Nakua kukusaidia."

### Aina za uokozi

Kumuokoa mtu ni hatari, na watu wengi huzama kila mwaka wakiwa wanajaribu kuwasaidia watu wengine majini.

Njia mbali mbali za uokozi zinaweza kutumika na mwalimu, na ni muhimu kwa mwalimu kuwa mahiri katika njia zote.

Uokozi wa nchi kavu:	Uokozi wa kuogelea:
<ul style="list-style-type: none"><li>• Uokozi wa kumfikia.</li><li>• Uokozi wa kurusha.</li><li>• Uokozi wa kukwamua.</li></ul>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Na kitu kinachoelea.</li><li>• Bila ya kitu kinachoelea.</li></ul>

## 2.4 Ujuzi wa uokoaji kwa walimu

### Uokoaji wa nchi kavu

Kufanya uokozi kutoka nchi kavu au maji yenye kina kifupi sana ni njia salama kabisa kwa walimu kwa vile haihitaji kuingia maji ya hatari au kuingiliana moja kwa moja na mtu anaezama. Kama mwalimu anafundishia kutoka nchi kavu na akagundua kuwa mwanafunzi ana matatizo, daima anapaswa kujaribu uokoaji wa nchi kavu kabla ya kuingia katika maji na kufanya uokozi wa kuogelea.

### Uokozi wa kumfikia

Wakati gani?	Wakati mtu aliye matatizoni yupo karibu na ufukwe.
Kwa nini?	Ni njia ya usalama zaidi ya uokoaji.
Vipi?	Fuata hatua 1, 2 na 3 chini.



#### Hatua ya 1

- Mfikie muhusika kwa kutumia kitu kirefu na kigumu, kama vile fimbo au gongo.

#### Hatua ya 2

- Kaa chini ili muhusika asiweze kukuvuta majini.



#### Hatua ya 3

- Mvute muhusika nje.

## 2.4 Ujuzi wa uokoaji kwa walimu


### Uokozi wa kurusha

Wakati gani?	Ikiwa mtu aliye matatizoni yuko karibu na ufukwe lakini sio karibu vya kutosha kuweza kumfanya uokozi wa kumfikia.
Kwa nini?	Hupunguza hatari kwa muokozi – hakuna haja ya kuogelea.
Vipi?	Fuata hatua 1, 2, 3 na 4 chini.



### Hatua ya 1

- Muite mtu aliye kwenye matatizo.



### Hatua ya 2

- Mrushie muhusika kitu kinachoelea kama vile kamba au geloni.



### Hatua ya 3

- Mwambie muhusika apige miguu na kuogelea kuelekea pembezoni.

### Step 4

- Msaidie muhusika kutoka majini.

## 2.4 Ujuzi wa uokoaji kwa walimu

### Uokozi wa kukwamua

<b>Wakati gani?</b>	Ikiwa mtu aliye matatizoni yuko karibu na ufukwe na katika maji yenye kina kifupi. Muhusika anaweza kuwa ameingia kwenye "shimo".
<b>Kwa nini?</b>	Hupunguza hatari kwa muokozi – Hakuna haja ya kuogelea. Haihitaji kitu kinachoelea.
<b>Vipi?</b>	Fuata hatua ya 1 na 2 chini.



#### Hatua ya 1

- Muite muhusika.
- Ingia majini kwa uangalifu, chukua fimbo/gongo kama itawezekana ili kuweza kupima kina cha maji na kwa muhusika kulishikilia.

#### Hatua ya 2

- Mpe muhusika upande mmoja wa fimbo/gongo.
- Mvute muhusika upande na msaidie kutoka nje ya maji.

## 2.4 Ujuzi wa uokoaji kwa walimu

### Uokozi wa kuogelea

Katika matokeo mengi mwalimu atakuwa majini wakati mwanafunzi atapopata matatizo, au mwanafunzi atakuwa mbali kuweza kufanyiwa uokozi wa nchi kavu. Uokoaji unaohitaji mwalimu kuogelea ni hatari zaidi kuliko uokozi wa nchi kavu kwa sababu:

- hatari ya maji
- wale wanaokolewa wanaweza kuchanganyikiwa na kumnyakuwa mwalimu.

Uokozi wa kuogelea ufanyike pale tu pasipokuwa na uwezekano wa kufanyika uokozi wa nchi kavu.

Inapowezekana, vifaa vinavoelea vya uokozi vitumike kumsaidia uokozi wa mtu mwenye fahamu. Hata hivyo, kama vifaa vya uokozi havipo – au mtu amepoteza fahamu – basi mwalimu awe na uwezo wa kumvuta muhusika ufukweni.

#### 1. Kuingia majini



Tambua alipo mtu aliye matatizoni kabla ya kuingia majini.



Kama kina cha maji hakijuulikani – au uwepo wa vitu chini ya maji haujulikani – basi kimbia hadi maji ya kifua kabla ya kuanza kuogelea.

#### 2. Kuogelea kwenda kwa mtu aliye matatizoni

Unapo ogelea kwenda kwa mtu aliye matatizoni, mwalimu lazima aogelee kifudi fudi, mara kwa mara anyanyue kichwa kuangalia alipo muhusika.

Mwalimu anapaswa awasiliane na muhusika ili ajue kuwa msaada unakuja.



## 2.4 Ujuzi wa uokozi kwa walimu

### 3. Kumkaribia mtu aliye matatizoni

Mtu aliye matatizoni anaweza kujaribu kumngangania mwalimu akiwa karibu. Anapowasili katika eneo la tukio, mwalimu aweke masafa salama baina yake na muhusika na kutathmini hali hiyo.



Kama mwalimu atakuwa na kifaa cha kuokolea, basi amrushie kifaa hichi muhusika huku akidumisha masafa salama baina yao.



Kama mwalimu hana kifaa cha kuokelea basi ajiweke katika mkao utakaoepusha kunganganiwa na muhusika, muweke chali na jitaarishe kumvuta ufukweni.


Hii hufanikiwa kwa mwalimu kumsogelea muhusika kwa nyuma.

### 4. Kumrudisha muhusika ufukweni

#### Kumvuta kwa kitu kinacho elea

Wakati kitu kinachoelea kinatumika kwenye uokozi, mwalimu anaweza kushikilia kifaa badala ya kumshikilia mtu moja kwa moja.

Mwalimu ashikilie kifaa kwa mkono mmoja na amvute muhusika upande.



## 2.4 Ujuzi wa uokozi kwa walimu

### Kumvuta bila ya kitu kinachoelea

Ambapo kitu kinachoelea hakijatumika kwa uokoaji, mwalimu itabidi amshikilie muhusika moja kwa moja ili kumvuta nyuma. Kuna njia mbali mbali za kumshikilia mtu aliye katika matatizo:

#### Msalaba wa kifua

Uvutaji wa msalaba wa kifua unamruhusu mwalimu kuwa na udhibiti wa muhusika na inafaa kutumika kumsaidia mtu aliyechanganyikiwa. Hii humpa muhusika hisia ya usalama kwa vile kichwa chao kipo nje ya maji, na yuko karibu kimwili na mwalimu.



- Mwalimu hupitisha mkono juu ya bega na kifua, na kumkamata muhusika chini tu ya kwapa.
- Mwalimu huweka bega la muhusika katika kwapa yake.
- Mwalimu hugeuka ubavuni ili nyonga yake iwe chini ya sehemu ya chini ya mgongo wa muhusika.



#### Funga kidevu

Uvutaji wa funga kidevu hutumika kuwapa msaada wa ziada watu walio katika matatizo. Inamruhusu mwalimu kuzungumza na kumfuatilia muhusika wakati akimpeleka ufukweni. Hii hutoa hisia ya usalama zaidi kwa muhusika na udhibiti zaidi kwa mwalimu.



- Akielekea kulala chali, mwalimu hupitia begani na kumkamata muhusika kidevuni.
- Mwalimu huweka mkono wa pili chini ya kwapa ya muhusika.
- Mwalimu huogelea na mkono mmoja na miguu, akimuweka muhusika chali.
- Mwalimu husogeza kichwa cha muhusika mabegani mwao na kumvuta ufukweni.



## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu



Matokeo ya kujifunza:

1. Kufahamu kanuni za huduma ya kwanza.
2. Kufahamu jinsi ya kutathmini majeruhi.
3. Kufahamu jinsi ya kutoa matibabu ya haraka kwa dharura mbali mbali za kiafya.

### Huduma ya kwanza ni nini?

Huduma ya kwanza ni huduma ya mpito na haraka anayopewa mtu aliyejeruhiwa au mgonjwa kabla ya kuanza kwa matibabu ya kitaalamu. Kuna sababu nyingi za kujeruhiwa wakati wa kujifunza kuogelea, hasa katika mazingira ya nje. Mwanafunzi anaweza:

- kujikata na kitu chenye ncha kali majini
- kuchomwa au kutafunwa na mnyama
- kuteleza na kujigonga kichwani
- kuzamia kwa muda mrefu.

Ingawa matokeo mengi yatahitaji matibabu madogo, mwalimu anatakiwa awe anaweza kutoa matibabu kwa majeraha madogo na makubwa, hasa kama ni kijijini.

### Kanuni za huduma ya kwanza

Kanuni kuu ya huduma ya kwanza ni:

- kuhifadhi maisha
- kumlinda muhusika na madhara zaidi
- kuzuwigia jeraha au maradhi kuzidi
- kutoa uhakika.

CPR ni ufupisho wa cardiopulmonary resuscitation na ni mbinu ya kufanya damu yenye oxygen kuzunguka mwilini kwa kukandamiza kifua na kutoa pumzi za uokozi. Katika matokeo machache hii huweza kurudisha mapigo ya moyo, na kubakisha shughuli za ubongo katika hali ya kawaida.

## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Tathmini

Ni muhimu kuwatathmini watu waliyo katika matatizo ile kujua ukubwa wa majeraha yao na hatua unazohitaji kuchukua ili kuwatibu. Katika matukio mengi utaweza kuona haraka tatizo ni nini na ortalitatua vipi. Hata hivyo, katika hali mbaya, ambapo mtu amepoteza fahamu, itabidi utizame na uhisi ili kufahamu nini tatizo na vipi ortalitatua.

### Tafuta chanzo cha hatari

Ni lazima mwalimu aangalie kwanza uwezekano wa hatari kabla ya kumkaribia na kumtathmini mtu aliye matatizoni.

### Angalia njia ya hewa, upumuaji na dalili za uhai

Ili mwili kufanya kazi unahitaji oksijeni. Hewa ina oksijeni. Wakati hewa inavutwa mwilini oksijini huingia kwenye damu kwa kupitia mapafuni. Oksijini kisha husambazwa mwilini na damu inayosukumwa na moyo.

Kama mtu hapumui kikawaida moyo wake unaweza ukasimama kufanya kazi. Ni muhimu sana kuweka njia ya hewa wazi, kuhakikisha upumuaji upo, na kuangalia dalili za uhai (kuhakikisha moyo bado unasukuma damu). Katika huduma ya kwanza vipaumbele hivi vinaitwa ABC:

- Airway (Njia ya hewa), Breathing (Upumuaji), Circulation (Mzunguko).

### Kama mtu amepoteza fahamu

#### Angalia njia ya hewa

Mavazi ya kubana kwenye njia ya hewa yalegezwe au yavuliwe.

Kama mtu amepoteza fahamu:

- fungua kinywa chake na toa uchafu wowote (pamoja na matapishi) kwa kumgeuza muhusika ubavuni
- inamisha kichwa nyuma kwa kuweka mkono juu ya paji la uso na vidole viwili chini ya kidevu.



#### Angalia upumuaji

Kama mtu amepoteza fahamu ni muhimu kuangalia kama anapumua kikawaida:

- sogeza shavy lako karibu na mdomo wao; sikiliza na hisi kama anapumua kwa sekunde 10
- angalia harakati za kifua.



Muhimu: Kutweta au upumuaji mdogo si upumuaji wa kawaida.

#### Cha kufanya akianza kutapika

Kama mtu ataanza kutapika, mgeuze ubavuni mara moja ili kupunguza uwezekano wa kupaliwa.

Ikiwezekana, tumia mkono wako kusaidia kichwa chao na vidole vyako kutoa kitu chochote kilichobaki kinywani.



## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Kama muhusika anapumua kikawaida

Kama muhusika anapumua kikawaida, unahitaji kuwaweka katika mkao mzuri ambao utaziweka njia za hewa wazi. Mueke muhusika katika mkao wa kupona ili:

- kuruhusu maji kutoka kinywani
- kumuweka muhusika katika hali ya utulivu wakati msaada ukitafutwa.

Kama watawekwa katika mkao mmoja kwa zaidi ya dakika 20 basi wanapaswa kugeuzwa upande mwengine.

#### Mkao wa kupona



#### Hatua ya 1

- Piga magoti kando na muhusika na hakikisha kuwa miguu yake yote imenyooka.
- Weka mkono ulio karibu na wewe katika nyazi 90 na mwili, pindisha kisugudi na elekeza kiganja cha mkono juu.



#### Hatua ya 2

- Lete mkono juu ya kifua, na shikilia nyuma ya mkono huo dhidi ya shavu la muhusika liliilo karibu na wewe.



#### Hatua ya 3

- Kwa mkono wako mwengine, kamata mguu wa mbali juu ya goti na uvute juu, ukiweka nyayo juu ya ardhi.
- Ukigandamiza mkono shavuni, vuta mguu ulio mbali ili kumgeuza muhusika kukuelekea wewe.

#### Hatua ya 4


- Rekebisha mguu wa juu mpaka nyonga na goti vipinde juzi 90.
- Inamisha kichwa nyuma ili kuhakikisha kuwa njia ya hewa inabaki wazi.
- Angalia upumuaji mara kwa mara.

## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Kama muhusika hapumui kikawaida

Kama hakuna dalili za upumuaji wa kawaida, ni muhimu kwako kumpumulia muhusika.

#### Ufunguaji wa njia za hewa na upumuaji wa awali



#### Hatua ya 1

- Inamisha kichwa nyuma inua kidevu kwa kutumia vidole viwili.
- Kwa mkono mmoja, bana pua kuzuia hewa kukimbia.

#### Hatua ya 2

- Fungua midomo ya muhusika na ziba kinywa chake kwa midomo yako.
- Puliza mpaka kifua kinyanyuke.
- Puliza tena kifua kitaposhuka.  
Rudia mara 5.
- Endela kuangalia dalili za uhai.

#### Angalia dalili za uhai (Mzunguko)

Baada ya kutoa pumzi mara 5 za mwanzo ni muhimu kujua kama moyo bado unafanya kazi na damu inazunguka mwilini.

Tumia sekunde 10 kuangalia dalili za uhai:

- Angalia kama muhusika anaitikia.
- Angalia harakati za mwili, haswa macho na vidole.
- Angalia kuwa anahisi maumivu kwa kumnyukua begani.

Kama kuna dalili za uhai muweke muhusika katika mkao wa kupona.




## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Kama hakuna dalili za uhai


Kama hakuna dalili za uhai, basi damu inahitajika kusukumwa mwilini na mwalimu.

### Ukandamizaji wa kifua



### Hatua ya 1

- Weka kisigino cha kiganja chako katikati ya kifua cha muhusika, baina ya chuchu.
- Kwa watu wazima, weka mkono wako wa pili juu ya mkono wa kwanza na viambatanishe vidole.



### Hatua ya 2

### Hatua ya 2

- Ukiweka mikono yako wima, na kwa kutumia uzito wa mwili wako, kandamiza kifua chake kiasi cha 5–6cm ndani.
- Rudia hivi mara 30 ukifanya takriban mikandamizo 2 kwa sekunde.

- Baada ya mikandamizo 30 mpumulie mara 2.
- Halafu mkandamize mara 30.
- Endelea na mzunguko huu mpaka muhusika atakaporudisha dalili za uhai, au katafute msaada baada ya dakika 30.

### Ukandamizaji kwa watoto

Kwa watoto (wenye umri wa takriban miaka 1-8) tumia mkono mmoja tu kukandamiza kifua kwa takriban moja ya tatu ya kina cha kifua.

Kama msaada wa haraka haukupatikana, mtu anatakiwa kwenda kuutafuta kwa wakati muafaka.

## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Kama mtu hajapoteza fahamu

Kama mtu hajapoteza fahamu na anapumua kikawaida, basi majeraha au magonjwa yanaweza kutibiwa. Kama huwezi kutoa matibabu au huna uhakika wa utaratibu sahihi basi mpeleke muhusika kwa wataalamu wa afya.

Yafuatayo ni baadhi ya majerahi na magonjwa ambayo unaweza kukutana nayo wakati ukifundisha kuogelea, na maelekezo ya jinsi ya kuyatibu:

#### Majeraha

Vidonda vilivywazi husababishwa na mambo mbali mbali ikiwa na pamoja na kukanya jiwe lenye makali na vigae vilivyoyunjika. Vidonda vinaweza kusababisha kutoka kwa damu nyingi. Mara baada ya njia ya hewa kuwa wazi na upumuaji wa kawaida umepatikana ni muhimu kuzuia umwagikaji wa damu na kutibu kidonda ipasavyo.

**Kumbuka:** Punguza kugusa damu kwa kutumia mifuko ya plastiki au glavu.

Kama uvujaji wa damu ni mkubwa ni muhimu kuzuia uvujaji mara moja.

- Kwa kutumia kipande cha nguo, kandamiza kwenye kidonda. Kwenye kidonda kidogo kiache kipande kwenye kidonda kwa dakika 10 kabla ya kuangalia kama uvujaji umesimama. Muhsika anaweza kukandamiza pia kupunguza uwezekano wa kuambukizana.
- Ikiwa damu itarovya kipande cha kwanza basi weka kipande cha pili juu yake.
- Kama inawezekana, nyanyua kiungo kupunguza mtiririko wa damu.
- Hakikisha muhsika ametulia.
- Pata msaada zaidi kwa wataalamu wa afya.



#### Kuna kitu kwenye kidonda?

Kama kidonda kina kitu kigeni (mfano kigae au kijiti), usikitoe. Funga kidonda bila ya kukandamiza moja kwa moja.

Kama inawezekana tafuta msaada zaidi kutoka kwa wataalamu wa afya.

## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Mifupa iliyovunjika

Kuvunjika kwa mifupa husababishwa na vishindo kama kuteleza kwenye mwamba. Mifupa iliyovunjika inahitaji kuchunguzwa na kutibiwa hospitali ili kuhakikisha inapona kikamilifu.

Kuna aina kuu mbili za kuvunjika:

Wazi – ambapo mfupa hupasua ngozi na huonekana.

- Zuia umwagikaji wa damu kama ilivyoolezwa kwenye kurasa ya 82.
- Jaribu kuweka kiungo kilichojaruhiwa kwenye utulivu.
- Mchukue muhusika hospitali kwa matibabu.

Funika – ambapo mfupa haupasui ngozi.

- Usijaribu kunyoosha kiungo.
- Weka kiungo kwenye hali tulivu.
- Mpeleke muhusika hospitali.


Ikiwa muhusika amevunjika mguu itakuwa muhimkuufungia mguu ili kuuzuulia usitikisike wakati wa kumsafirisha muhusika kwenda hospitali. Kukifungia kiungo huzuia kutikisika na kuzidisha maumivu. Vijiti na kamba vinawenza kufanya banzi ya kutosha kuweka kiungo mahala pake (tizama kulia). Tumia kamba kuambatanisha vijiti vilivyonjooka mguuni. Ikiwezekana, tumia vijiti wiwili kuunyoosha mguu. Vifaa vyengine vinawenza kutumika pia. Kama nyenzo zinazofaa za kutengenezea banzi hazikupatikana, basi mguu mwengine unaweza kutumika kuunyoosha mguu uliojeruhiwa.



### Uvujaji wa damu puani

Mambo mengi yanaweza kusababisha kuvuja damu puani. Hata hivyo, wakati ukifundisha kuogelea mara nyingi hutokezea pale watu wawili wanapogongana. Mueke muhusika chini na muinamishe mbele kuhakikisha kuwa damu haizibi koo. Weka kichwa juu ya moyo.

- Weka kitu baridi, kilichorowa puani kupunguza upitaji wa damu.
- Bana pua.
- Angalia kama uvujaji wa damu umeisha baada ya dakika 10 na kandamiza.
- Kama uvujaji wa damu haujesha baada ya dakika 30, mpeleke mgonjwa hospitali.



## 2.5 Ujuzi wa huduma ya kwanza kwa walimu

### Kutafunwa na mnyama

Jerah linaweza kusababishwa na kutafunwa na wanyama, kwa mfano nyoka au mbwa katika eneo la kufundishia.

Kuumwa na wanyama wenye sumu, au wenye maradhi, inaweza kumfanya muhusika kutokuweza kupumua au kuvuja damu nyingi. Kabla ya kutibu majeraha ya kuumwa, hakikisha mnyama hawezi kushababishwa madhara zaidi kwa wanafunzi au mwalimu.

Mwalimu anatakiwa kuepuka kugusa sumu au mate kwa kutumia kizuizi (kama vile mfuko wa plastiki au jani la mgomba).

### Kutafunwa na nyoka

Kama unatuhumu kuwa muhusika ametafunwa na nyoka, ni muhimu kupunguza mzunguko wa sumu mwilini. Punguza harakati za muhusika.

- Mlaze muhusika na mpe moyo.
- Ondoa pete au vizuizi vyovyote kwa sababu sehemu iliyoumwa inaweza kuvimba.
- Mpeleke muhusika hospitali.
- Usijaribu kufonza damu au kumkata muhusika ili kuiwacha damu ivuje.

Kama nyoka bado yuhai, usijaribu kumuwa kwa kuwa anaweza kuwa ni wa hatari.

Kama nyoka alishauliwa, achukuliwe hospitali na muhusika ili atambuliwe. Hata hivyo, usimkamate nyoka kwa mikono mitupu kwa sababu hata kichwa kilichojeruhiwa kinaweza kukutafuna!

### Kutafunwa na mbwa

Kuumwa na mbwa kunaweza kusababishwa uvujaji mkubwa wa damu au maambukizo ya maradhi.

Kichaa cha mbwa ni tatizo mashuhuri katika nchi nyingi na ni muhimu kwa walimu kuto kuiweka wao au wanafunzi wao kwenye hatari ya kuambukizwa ugonjwa huu.

- Hakikisha mnyama hawezi kusababishwa hatari tena.
- Ondoa pete au kizuizi chochote kwa sababu sehemu iliyoumwa inaweza kuvimba.
- Osha kidonda vizuri kwa maji safi kwa dakika 15. Tumia maji yanayotiririka kama inawezekana.

Kama maji yanayo tiririka hayapatikani basi badilisha mara kwa mara maji yanayotumika kusafishia kidonda. Usiguse kidonda.

- Kifunge kidonda kwa kitambaa kikavu.
- Kama kidonda kinavuja damu sana basi toa tiba kama ilivyolezwa kwenye ukurasa wa 82.

Kama muhusika ataonyesha dalili za maambukizi basi mpeleke hospitali. Ishara na dalili za maambukizi ni pamoja na:

- maumivu kwenye kidonda
- wekundu na uregevu
- kuvimba
- usaha au belaghami.

## 2.6 Mahitaji ya kufundishia



Matokeo ya kujifunza:

1. Kufahamu ujuzi wa msingi.
2. Kufahamu maendeleo kuititia ujuzi wa msingi.
3. Kufahamu haja ya kuweka rekodi ya tathmini.

### Ujuzi wa msingi

Kuna ujuzi 9 ya msingi ambayo mwanafunzi lazima ajifunze ili kufikia uwezo wa Kujikoa na Uokoaji. Ujuzi huu wa msingi unaweza kugawanywa katika sehemu 3:

**Sehemu ya 1: Maandalizi**

**Sehemu ya 2: Mapigo**

**Sehemu ya 3: Msaada**

### Maandalizi

1. Kuingia/kutoka – mwanafunzi anaweza kuingia na kutoka majini kwa usalama.
2. Mwendo – mwanafunzi anajiamini kutembea majini.
3. Upumuaji – mwanafunzi ana uwezo wa kudhibiti upumuaji wao.

### Mapigo

4. Kuelea – mwanafunzi ana uwezo wa kuelea majini chali na kifudifudi.
5. Kujisukuma na kunyinyirika – mwanafunzi anajiamini kunyinyirika majini.
6. Mateke – mwanafunzi ana jiamini kupiga miguu yao chali na kifudi fudi.
7. Mikono na miguu – mwanafunzi anajiamini kutumia mikono yao kuogelea.

### Msaada

8. Kujikoa – mwanafunzi anaweza kujikoa.
9. Kuwaokoa wengine – mwanafunzi anaweza kufanya uokozi wa nchi kavu.

## 2.6 Mahitaji ya kufundishia

### Kufundisha ujuzi wa msingi

Sehemu ya Kujiokoa na Uokoaji imegawanjwa katika sehemu 15, kila moja ikiwa na matokeo maalum. Ni muhimu matokeo yote yapatikane kabla ya kwenda hatua nyengine.

Kila somo lichukue takriban dakika 90 na lazima liwe na mapumziko baada ya takriban dakika 45. Masomo yanaweza kufundishwa katika kipindi kifupi, au katika kipindi kirefu. Ni wajibu wa mwalimu kuhakikisha kuwa wanafunzi wako mahiri katika ujuzi wote unaohitajika kufaulu tathmini ya mwisho.

### Maendeleo

Kuna masomo 15, ambayo yamegawanywa katika hatua tatu, pamoja na tathmini:

Hatua ya	Masomo	Maelezo
1. Mwanzo	1, 2, 3, 4, 5	Wanafunzi wanafundishwa kwa msaada wa moja kwa moja kutoka kwa mwalimu au mwanafunzi mwenzake.
2. Kati	6, 7, 8, 9	Wanafunzi hufanya mazoezi kwa msaada wa kitu kinachoelea.
3. Mwisho	10, 11, 12, 13, 14	Wanafunzi hufanya mazoezi bila ya msaada.
Tathmini	15	Wanafunzi hupewa muda wa kujaribu ujuzi wao na kukamilisha tathmini rasmi.

Katika kila hatua (mbali na Tathmini), kila somo lina ujuzi wa misingi 3 – Maandalizi, Mapigo na Msaada. Masomo yote katika kila hatua ni lazima yakamilike kabla ya kuingia kwenye hatua inayofuata.

### Usajili

Ni muhimu kuchukua mahudhurio mwanzo wa kila somo. Hii ni kuhakikisha kuwa:

- unajua una wanafunzi wangapi katika kila somo
- unajua kama mwanafunzi amekosa somo
- kuwa na rekodi ya jumla ya wanafunzi uliofundisha.

### Tathmini

Wanafunzi wafanyiwe tathmini mara kwa mara ili kuhakikisha wanafikia malengo ya kila somo.

Mwisho wa mafunzo tathmini rasmi itafanywa kuhakikisha wanafunzi wana uwezo wa:

- kuogelea mfululizo
- kuelelea chali
- kupiga miguu wakiwa chali
- Kuelela wima
- kuonyesha uokozi wa nchi kavu
- kugeuka kutoka chali kwenda kifudi fudi, na kifudi fudi kwenda chali.

## 2.6 Mahitaji ya kufundishia

Vtendo	Mwanzo				Kati				Mwisho					
	Somo la 1	Somo la 2	Somo la 3	Somo la 4	Somo la 5	Somo la 6	Somo la 7	Somo la 8	Somo la 9	Somo la 10	Somo la 11	Somo la 12	Somo la 13	Somo la 14
Kuingia/ kutoka	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	Onyesha uin-giaji na utokaji salama	
Mwendu	Mkanate mwenzio, tembea na kimbia kwenye maji ya kifua.	Mkanate mwenzio, chupa kwenye maji ya kifua	Mkanate mwenzio, chupa kwenye maji ya kifua	Mkanate mwenzio, chupa kwenye maji ya kifua	Mkanate kitu kinachoelea, tembea na kimbia kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	Mkanata kitu kinachoelea, chupa chupa kwenye maji ya kifua	
Upumujii	Osha uso na nywele majini	Toa pumzi majini	Puliza kitu kinachoelea juu ya maji	Zamisha uso majini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Gusa chini nara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	Kaa chini mara kadhaa huku ukitoa pumzi	
Kuelea			Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	Elea Chali ukisaidiwa na mwalimu, halafu kanyaga chini	
Sukuma na nyinyika			Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	Sukuma na unyinyirike fudi ukisaidiwa na mwalimu.	
Mateke	Wekamikono chini, piga miguu chali	Mikono na miguu	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	Piga miguu chali	
Mikono/ mikono na miguu			Piga mikono hukuu ukisaimama majini											
Kuijokoa														
Kuwaokoa wengine			Piga kelele na uite msada											

## 2.6 Mahitaji ya kufundishia

## Fomu ya mahudhirio na tathmini

## 2.7 Mpangilio wa somo

### Somo 1

#### Matokeo ya kujifunza

- Kuwa na ufahamu mzuri wa Ujumbe wa Usalama Majini.
- Kuwa na uwezo wa kuonyesha uingiaji na utokaji salama ukisaidiwa.
- Kuweza kutembea na kukimbia kwenye maji ya kifua bila ya tabu ukisaidiwa.
- Kuweza kutia maji usoni na nyweleni bila ya tabu.
- Kuweza kupiga miguu kwenye maji yenye kina kidogo bila ya tabu.

#### Nyenko

Ujumbe wa Usalama Majini.  
Kadi.  
Magongo marefu.

### Ujumbe wa Usalama Majini

Muda: dakika 35

Lengo: Wanafunzi wawe na ufahamu mzuri wa Ujumbe wa Usalama Majini.

Kabla ya wanafunzi kuingia majini, wafundishe ujumbe 10 muhimu ya usalama majini (angalia kurasa 19–48):

#### Itambue hatari

1. Jua hali ya maji na hali ya hewa kabla ya kuingia majini.
2. Pima kina cha maji na hatari zilizopo chini ya maji kabla ya kuingia majini.
3. Tambua uwepo wa wanyama.

#### Jiweke salama

4. Kamwe usiingie majini peke yako.
5. Tii alama za usalama na bendera za onyo.
6. Tambua jinsi gani na wakati gani wa kutumia koti la kuokolea maisha.
7. Daima mwambie mtu lini na wapi unapokwenda pembezoni mwa maji.

#### Waweke wengine salama

8. Jifunze njia salama ya kuwasaidia wengine bila ya kujiweka wewe hatarini.
9. Daima simamia watoto ndani au pembezoni mwa maji.
10. Weka nyumba yako salama.

### Kuweka kanuni

Muda: dakika 5


Weka kanuni za tabia:

- Daima msikilize mwalimu.
- Usikimbie.
- Usipigane.
- Daima fanya ulichoambiwa ufanye – usifanye kitu chochote mpaka uambiwe ufanye hivyo.

## Kuingia/kutoka

Muda: dakika 10

Kuingia upande wenye kina: hutumika kuingia majini upande wenye kina kirefu.



### Hatua ya 1

- Ukiwa umekaa weka mikono yote miwili upande mmoja wa mwili wako.

### Hatua ya 2

- Geuka kitumbo tumbo.
- Taratibu shusha mwili wako majini ukitanguliza miguu.
- Shikilia upande au simama.

Kuingia mteremkoni: Hutumika kuingia majini kwenye mteremko.






### Hatua 1

- Tafuta fimbo ndefu.
- Tumia fimbo kuchocha chini, ukiangalia mashimo mbele yako.

### Hatua 2

- Sogea mbele taratibu, huku ukiendelea kuangalia mashimo.

Kutoka upande wenye kina: hutumika kutoka kwenye upande wenye kina.



#### Step 1

- Place hands, shoulder-width apart and jump up so your weight is on your hands.

#### Step 2

- Place stomach on the side.

#### Step 3

- Rotate into a seated position.

## Mwendo

## Muda: dakika 10

Temebe na kimbia majini

Kina cha maji: kiunoni–kifuani

Lengo: Kuweza kutembea na kukimbia kwenye maji ya kifua bila ya tabu kwa kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi hutumia wanafunzi wenzao kuwasaidia.

- Wapange mstari wanafunzi sambamba na ufukwe kwenye maji ya kiunoni.
- Watembeze wanafunzi sambamba na ufukwe.



## Hatua ya 1

- Tafuta mwenzio.
- Weka mikono yote miwili kwenye mabega ya mtu aliye mbele yako.

## Hatua ya 2

- Panga mstari na tembea taratibu, ukimfuata mtu aliye mbele yako.

- Pale wanafunzi wanapozidi kujiamini, ongeza mwendo na kina cha maji.
- Waamrishe wanafunzi waliombele kubadilisha mwelekeo.


## Upumuaji

Muda: dakika 15

Kuzuia pumzi

Kina cha maji: nchi kavu

Lengo: Fanya mazoezi ya kuvuta na kuzuia pumzi.  
 Msaada: Shughuli hii hufanywa nje ya maji.




## Hatua ya 1

- Vuta pumzi nydingi.
- Rudia uziaji wa pumzi mpaka wanafunzi watapoweza kuzuia pumzi kwa sekunde 10 bila ya tabu

Osha uso na nywele majini

Kina cha maji: kiunoni

Lengo: Kuweza kuosha uso na nywele majini bila ya tabu.  
 Msaada: Wanafunzi wasimame kwenye duara wakishikana mikono kwa msaada.



## Hatua ya 1

- Simama kwenye duara.
- Shika mkono wa mtu aliye pembezoni mwako.

## Hatua ya 2

- Osha uso na nywele majini.
- Hakikisha unaufunika uso wote na maji!

- Taratibu ongeza muda wa kuendelea kushikana mikono baada ya kutoa uso majini. Hii huwapa moyo wanafunzi kutokufuta maji usoni kila wakati wanapoingiza uso wao majini.



### Mateke

Time: 15 minutes

Mateke ukiwa chali

Kina cha maji: magotini

- Lengo: Kuweza kupiga miguu wakiwa chali katika maji ya kina kifupi bila ya tabu.
- Msaada: Wanafunzi wajisaidie wenyewe kwa kutumia mikono.



### Hatua ya 1

- Chutama kwenye maji ya kina kifupi na weka visugudi vyako chini.
- Inamia nyuma majini.
- Nyoosha miguu yako na inyanyue isiguse chini.

- Wahamasisha wanafunzi kuangalia miili yao ili kuhakikisha miguu yao imenyooka na vidole vimefanya ncha.
- Washirikishe wanafunzi kwa kuwashamasisha kufanya mialiko mikubwa iwezekanavyo.

### Hatua ya 2

- Piga miguu yako kwa kupishana.
- Piga kutokea kiunoni.
- Endelea kuinyoosha miguu na kuilegeza.
- Weka magoti yako chini ya maji.

## Somo la 2

### Matokeo ya kujifunza

- Kuwa na uwezo wa kuonyesha jinsi ya kuingia na kutoka salama majini kwa kusaidiwa.
- Kuweza kuruka ruka kwenye maji ya kifua kwa kusaidiwa.
- Kuweza kutoa pumzi majini
- Kuweza kuelea kwa mbele kwa sekunde 10 na kuweza kusimama baada ya hapo kwa kusaidiwa.
- Kuweza kujisukumu na kunyinyirika kwa mbele kwa kusaidiwa.
- Kuweza kupiga miguu kifudi fudi kwa sekunde 10.
- Kuweza kuonyesha jinsi ya kupiga mikono wakati umesimama.
- Kufahamu kanuni za msingi za uokozi wa sauti na ishara.

### Nyenko

Long sticks.

## Weka kanuni


## Muda: dakika 2

Weka kanuni za tabia.

## Kuingia/kutoka

## Muda: dakika 3


Kuingia upande wenye kina:  
hutumika kuingia kwenye  
upande wa maji yenye kina.



Kuingia kwenye mteremko:  
hutumika kuingia kwenye  
maji yenye mteremko.



Kutoka kwenye upande wenye kina:  
hutumika kutoka kwenye maji  
yenye kina.





## Mwendo

Muda: dakika10

Lengo: Kuweza kuchupachupa kwa miguu miwili na mmoja kwa kusaidiwa.  
 Msaada: Waweke wanafunzi wawili wawili na waombe wakamatane mikono kwa msaada.

Ruka majini

Kina cha maji: kiono - kifuani



## Hatua ya 1



- Tafuta mwenza na umshike mikono yake yote miwili.
- Chutama chini katika mkao wa kukaa.

## Hatua ya 2

- Jisukume juu kwa miguu yote ili miguu yote iachie ardhi.
- Jaribu kuweka miguu yote chini kwa wakati mmoja.

Chupa chupa majini

Kina cha maji: kiuno – kifuani



## Hatua ya 1

- Tafuta mwenza na umkamate mkono.
- Nyanya mguu mmoja na simamia mguu mmoja.

## Hatua ya 2

- Jaribu kuruka ulipo kwa kutumia mguu mmoja.

- Pale wanafunzi wanapozidi kujiamini, hatua kwa hatua ongeza kina cha maji kutoka kiunoni kwenda kifuani.
- Rudia zoezi kwa kusonga mbele, nyuma na pembedi majini.



## Upumuaji

Muda: dakika10

Toa pumzi majini

Kina cha maji: kifuani

Lengo: Kuweza kutoa pumzi majini  
 Msaada: Wanafunzi wasimame kwenye duara wakikamatana mikono kwa msaada.



## Hاتua ya 1

- Weka kidevu chako ndani ya maji.
- vuta pumzi nyingi.

- Rudia utaratibu huu hadi wanafunzi watapuweza kutia midomo yao majini bila ya tabu.

## Hاتua ya 2

- Ingiza mdomo wako majini na toa pumzi mdomoni.

## Burudika!

Hamasisha wanafunzi:

- kuliza sauti kama mashine ya boti
- kuangalia mabofu mangapi wanapuliza



## Kuelea

Muda: dakika10

Kuelea kifudi fudi

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kuelea kwambele kwa sekunde 10 na kusimama baada ya hapo kwa kusaidiwa.
- Msaada: Mwanafunzi amkamate mikono iliyonyooshwa ya mwalimu au mwenza. Mwalimu au mwenza awe amechutama kina cha mabega.



## Hatua ya 1

- Nyoosha mikono yako mbele.
- Vuta pumzi kwa wingi.



## Hatua ya 2

- Ingiza uso wako majini.
- Nyoosha miguu yako.
- Toa pumzi.

## Hatua ya 3

- Unapoishiwa na pumzi kunja magoti kifuani, nyanyua kichwa, kandamiza mikono ya mwalimu na weka miguu yako chini.




## Sukuma na unyinyirike

Muda: dakika15

Sukuma na unyinyirike mbele


Kina cha maji: kiunoni–kifuani

- Lengo: Kuweza kusukuma na kunyinyirika mbele kwa kusaidiwa.
- Msaada: Mwalimu au mwenza atasimama mbele ya mwanafunzi. Mwanafunzi atajisukuma mbele na atanyinyirika kwenye mikono ya mwalim/mwenza.



## Hatua ya 1

- Nyoosha mikono yako juu ya kichwa.
- Zzia pumzi zako.
- Inama mbele.
- Ingiza uso wako majini.



## Hatua ya 2

- Inama mbele na sukuma kwa nguvu kwa vidole ili mwili wako unyinyirike majini na miguu yako ielee.
- Pumua kwenye maji wakati unanyinyirika
- Kaa hivyo hivyo mpaka mwili wako utaposimama au utapoishiwa na pumzi.

## Hatua ya 3

- Ukisimama au kuishiwa na pumzi kunja magoti yako kifuani na weka miguu yako chini.

### Mateke

### Muda: dakika 15

Kupiga miguu kifudi fudi



Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kupiga miguu kifudi fudi kwa sekunde 10 kwa kusaidiwa.
- Msaada: Wanafunzi wakamate mikono iliyonyooshwa ya mwalimu au mwenza. Mwalimu au mwenza achutame kina cha mabega.



#### Upumuaji:

- Wanafunzi wahamasishwe kutoa hewa wakati uso wao ukiwa majini, na wanyanyue mdomo wao nje ya maji kupumua.



### Hatua ya 1

- Nyoosha mikono yako mbele.
- Nyanya miguu yako.
- Vuta pumzi nyingi iwezekanavyo
- Ingiza uso wako majini.

### Hatua ya 2


- Piga miguu yako kwa kupishana.
- Piga kuanzia kiunoni.
- Inyooshe miguu yako na ilegeze.
- Puliza kwenye maji wakati unapiga miguu,

## Mikono

## Muda: dakika10

Piga mikono ukiwa bado umesimama

Kina cha maji: kiunoni



### Hatua ya 1

- Simama wima / chuchumaa majini wakati umewe kidevu chako juu ya maji
- Weka videle vyako pamoja
- Nyoosha mkono wako mbele kwa umbali unaoweza.

### Hatua ya 2

- Vuta mkono wako nyuma kuelekea kifuani kwako.
- Plga mikono kwa kupishana.

#### Burudika!

- Waambie wanafunzi wajifanye kama wanaingiza chakula kwenye mdomo ulokuwepo juu ya kifua chao!

## Kuwaokoa wengine

Muda: daika 15

Piga kelele na ashiria

**Kina cha Maji : maji ya kifuani**

Kama mtu amechanganyikiwa majini basi kumpa maelezo yaliyo wazi inaweza kutosha kumsaidia kumfikisha nchi kavu.

- |                     |  |
|---------------------|--|
| Lengo:<br>ishara za | Kuwa na uwezo wa kufahamu kanuni za msingi za kupiga kelele na kutoa uokozi. |
| Msaada:             | Wanafunzi kufanya zoezi bila ya msaada.                                      |

- Waweke wanafunzi wawili wawili, mmoja akisimama katika maji ya kiunoni akijifanya kama mtu aliye katika matatizo na mwengine akisimama nchi kavu.
- Mawasiliano yaliyo wazi ni muhimu katika uokozi wowote. Waambie wanafunzi kufanya mazoezi kwa kutumia sauti na ishara za mikono kumhamasisha mtu kufika nchi kavu.



### Hatua ya 1

- Piga kelele kuita msaada(kama inawezekana muite mtu mzima).
- Muite mtu aliye majini.

### Hatua ya 2

- Tumia sauti yako na ishara za mikono kumhamasisha muhusika kuogelea hadi nchi kavu.

#### Burudika!

- Weka mashindano ya nani ataita msaada kwa kelele zaidi!

## Somo la 3

### Matokeo ya kujifunza

- Kuweza kuonyesha kuingia na kutoka salama kwa kusaidiwa.
- Kuweza kuweka kidevu majini na kupuliza kitu kinachoelea juu ya maji bila ya tabu.
- Kuweza kuelea chali kwa sekunde 10 na kuweza kusimama baada ya hapo kwa kusaidiwa.
- Kuweza kujisukuma na kunyinyirika chali kwa kusaidiwa.
- Kuweza kupiga miguu chali kwa sekunde 10 kwa kusaidiwa.
- Kuweza kugeuka kutoka kifudi fudi kwenda chali kwa kusaidiwa.

### Nyenko

- Long sticks.
- A floating object for each student.

## Weka kanuni


## Muda: dakika 2

Weka kanuni za tabia.

## Kuingia/kutoka

## Muda: dakika 3


Kuingia upande wenyе kina:  
hutumika kuingia kwenye  
upande wa maji yenye kina.



Kuingia kwenye mteremko:  
hutumika kuingia kwenye  
maji yenye mteremko.



Kutoka kwenye upande wenyе kina:  
hutumika kutoka kwenye maji  
yenye kina.





## Upumuaji

Muda: dakika 10

Puliza kitu kinachoelea juu ya maji

Kina cha maji: Kifuani

- Lengo: Kuweza kuweka kidevu majini na kupuliza kitu kinachoelea juu ya maji.  
 Msaada: Mwanafunzi ashike mkono wa mwenza kwa msaada itapobidi.



## Hatua ya 1

- Weka kidevu chako majini.
- Vuta pumzi kwa wingi.

## Hatua ya 2

- Fanya mazoezi ya kupuliza kitu kinachoelea majini.

## Burudika!

- Weka sehemu ya kuanzia na kumalizia.
- Waambie wanafunzi waweke kitu kinachoelea sehemu ya kuanzia na wakipulize haraka iwezekanavyo mpaka sehemu ya kumalizia.
- Atakaemaliza mwanzo ndio mshindi!


## Kuelea

Muda: dakika 15

Kuelea chali

Kina cha maji: kiunoni

- Lengo: Kuweza kuelea chali kwa sekunde 10 na baada ya hapo kusimama kwa kusaidiwa.
- Msaada: Mwalimu au mwenza atoe msaada chini ya mabega, akisimama nyuma na ubavuni kwa mwanafunzi. Mwalimu au mwenza achutame kina cha mabega. Hatua kwa hatua punguza kiasi cha msaada unachotowa.



## Hatua ya 1

- Lala chali majini.
- Laza kichwa chako nyuma ili uweze kuona uso wa mwalimu.
- Hakikisha masikio yako, yapo chini ya maji.

## Hatua ya 2

- Nyanyua tumbo lako.
- Nyoosha miguu yako na fanya ncha kwa vidole.
- Tanua mikono yako.
- Jiregeze na tulia majini.

## Burudika!

- Wahamasishe wanafunzi kulaza kichwa nyuma majini na kuhisabu ndege!

## Kujisukuma na kunyenyerika


Muda: dakika 15

Kujisukuma na kunyenyerika chali

Kina cha maji: kiunoni

Lengo: Kuweza kujisukuma na kunyenyerika chali kwa kusaidiwa bila ya tabu.

Msaada: Mwalimu au mwenza asimame nyuma na ubavuni mwa wanafunzi na uwasaidie chini ya bega. Kama inawezekana weka mkono mmoja chini ya mgongo.



## Hatua ya 1

- Simama katika maji ya kiuno.
- Weka mikono yako pembedi.

## Hatua ya 2

- Lala chali kwenye maji na jisukume kwa nguvu kwa vidole vyako ili mwili wako unyenyerike majini na miguu yako ielee.
- Nyoosha miguu yako.
- Tulia hadi mwili wako utaposimama.




## Kupiga miguu

Muda: dakika 15

Kupiga miguu chali

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuwa na uwezo wa kupiga miguu chali kwa sekunde 10 kwa kusaidiwa.
- Msaada: Mwalimu au mwenza atoe msaada chini ya mabega, akisimama nyuma na pembezoni mwa mwanafunzi. Mwalimu au mwenza achutame kina cha mabega.



### Hatua ya 1

- Nyanyua miguu yako.
- Nyanyua tumbo lako.
- Inamisha kichwa nyuma ili masikio yako yawe ndani ya maji.

### Hatua ya 2

- Piga miguu yako kwa kupishana.
- Piga kwa kuanzia kiunoni.
- Nyoosha miguu yako na ilegeze.
- Weka magoti yako chini ya maji.

## Kujiokoa

Muda: dakika 15

Kugeuka kutoka kifudi fudi kwenda chali

Kina cha maji: kifuani

Kuweza kujigeuza kutoka kifudi fudi kwenda chali  
huwaruhusu wanafunzi kupumzika chali wanapochoka  
kuogelea.

- Lengo: Kuweza kugeuka kutoka kifudi fudi kwenda chali kwa kusaidiwa.  
Msaada: Mwalimu au mwenza kusimama nyuma na ubavuni mwa manafunzi.



### Hatua ya 1

- Elea kifudi fudi majini.
- Geuza kichwa chako ubavu mmoja



### Hatua ya 2

- Tumia mkono wako kujizinguusha mwilimzima sambamba na kugeuza kichwa chako
- Endelea kuzunguka mpaka utapokuwa chali.

### Hatua ya 3

- Regeza mwili wako majini.
- Elea chali.
- Pumua pole pole.

## Mapitio na mazoezi

Muda: dakika 15

- Pitia somo la 3.
- Wanafunzi watumie muda kufanya mazoezi wanayohitaji.

## Somo la 4 & 5 – Mazoezi

Muda: dakika 90

### Maandalizi

#### Weka kanuni

Weka kanuni za tabia.

#### Kuingia/kutoka

Wanafunzi waweze kuonyesha kuingia/kutoka majini salama kwa kusaidiwa.

#### Mwendo

Wanafunzi waweze kutembea majini bila ya tabu kwa kusaidiwa na wenziwao.

#### Upumuaji

Wanafunzi waweze kuweka nyuso zao majini na kutoa pumzi.

### Mapigo

#### Kuelea

Wanafunzi waweze kuelea kifudi fudi na chali kwa sekunde 10 kwa kusaidiwa.

#### Kujisukuma na kunyenyereka

Wanafunzi waweze kujisukuma na kunyenyereka kifudi fudi na chali kwa kusaidiwa.

#### Mateke

Wanafunzi waweze kupiga miguu kifudi fudi na chali kwa sekunde 10 kwa kusaidiwa.

#### Mikono

Wanafunzi waweze kuonyesha kupiga mikono wakiwa wamesimama.

### Msaada

#### Kujiokoa

Wanafunzi waweze kujigeuza kutoka kifudi fudi kwenda chali kwa kusaidiwa.

#### Kuwaokoa wengine

Wanafunzi waweze kufahamu kanuni za msingi za uokozi wa kupiga kelele na kuashiria.

### Somo la 6

#### Matokeo ya somo

- Kuweza kuingia na na kutoka salama bila kusaidiwa.
- Kuweza kutembea na kuruka kwenye maji ya kifua na kitu kinachoelea.
- Kuweza kuruka na kuzama kwenye maji huku wakitoa pumzi.
- Kuweza kupiga kasia kwa mikono majini huku akitembea na kitu kinachoelea.
- Kuweza kuelewa wima kwa kutumia miguu pekee huku akishikilia kitu kinachoelea.
- Kuelewa kanuni za msingi za uokoaji wa kufikia.

#### Vifaa

- Fimbo ndefu.
- Vyombo vinavyoolea.
- Kamba.

### Weka sheria


### Muda: dakika 2

Weka kanuni za adabu.

### Kuingia/kutoka

### Muda: dakika 3


Kuingia upande wenye kina:  
hutumika kuingia kwenye  
upande wa maji yenye kina.



Kuingia kwenye mteremko:  
hutumika kuingia kwenye  
maji yenye mteremko.



Kutoka kwenye upande wenye kina:  
hutumika kutoka kwenye maji  
yenye kina.



## Mwendo

## Muda: muda10


Kutembea na kukimbia majini

Kina cha maji: kifuani

Lengo: Kuweza kutembea na kukimbia kwenye maji ya kifua na kitu kinachoelea.

Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mikono miwili, ikisha kwa mkono mmoja.

- Wapange wanafunzi sambamba na ukingo, maji ya kifuani.
- Waongoze watembee sambamba na ukingo wa maji.



## Hatua ya 1

- Shikilia kitu kinachoelea kwa mikono miwili.

## Hatua ya 2

- Panga mstari na tembea mbele pole pole, ukimfuata mtu aliye mbele yako.

- Wanafunzi wakijiamini zaidi, ongeza kasi ya mwengo na kina cha maji.
- Muelekeze mwanafunzi aliye mbele kubadili muelekeo.

Upumuaji



Muda: dakika 10

Zamisha kichwa majini mara kadhaa

Kina cha maji: kifuani



Lengo: Kuweza kuzamisha kichwa majini huku ukitoa pumzi kidogo kidogo.  
Rudia tena.

Msaada: Wanafunzi wasimame kwa umbo la duara huku wakishikana mikono  
kusaidiana au wasimame na mwenza.



### Hatua ya 1

- Vuta pumzi nyingi.



### Hatua ya 2

### Hatua ya 2

- Zamisha kichwa majini
- Toa pumzi kidogo kidogo hadi ziishe.

- Ukiishiwa pumzi,  
toa kichwa chako nje ya maji  
na vuta pumzi nyingi.

### Hatua ya 4

- Zamisha kichwa majini.
- Toa pumzi kidogo kidogo hadi ziishe.
- Rudia hatua hizi mara kadhaa.

## Mikono

## Muda: dakika15

Kupiga mikono huku ukitembe

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kupiga mikono majini huku ukitembe na kitu kinachoelea, ukizamisha uso majini.
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mkono mmoja, na mkono mmoja ukiwa umenyooshwa



- Wapange wanafunzi kwenye mstari sambamba na ukingo, maji ya kifuani.



## Hatua ya 1

- Vuta pumzi nyingi.
- Zamisha uso wako majini.
- Tembea ndani ya maji.
- Vikutanishe vidole vyako vya mikono.
- Nyoosha mkono wako mtupu na usogeze mbele kadri uwezavyo.

## Hatua ya 2

- Vuta mkono wako karibu na kiwiliwili chako.
- Sukuma maji nyuma yako.
- Rudisha mkono wako kupitia juu ya maji na rudia tena.
- Nyanyua kichwa chako ukihitaji kuvuta pumzi.

- Ikiwa mwanafunzi atakuwa anapata shida kuweza kutoa mikono juu ya maji, mwambie apige mikono hata ndani ya maji na anyanyue kichwa chake kwakutaka kupumua.
  - Wanafunzi wakijiamini, weka kitu kinachoelea kwenye mkono mwengine.
  - Wanafunzi wakijiamini zaidi, ongeza kasi ya mwengo na badili muelekeo.
  - Wahimize wanafunzi kupumua kwa kugeuza vichwa vyao upande.

## Kujiokoa

Muda: dakika 20

Kuelea wima kwa miguu pekee

Kina cha maji: juu ya kifua

Kuelea wima ni mbinu inayoweza kutumiwa na mtu aliye matatizoni majini kuelea kwa wima na kichwa kikiwa nje ya maji. Hii inawasaidia kupumzika, na kutumia mdomo kuomba msaada na kupunga mkono.

- Lengo: Kuweza kuelea wima majini kwa kutumia miguu pekee huku ukishikilia kitu kinachoele
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mikono miwili, na kunyanya miguu yote miwili.



## Hatua ya 1

- Weka kichwa chako juu nje ya maji.
- Elea ukiwa wima.
- Piga miguu yako mbele na nyuma kama unaendesha baiskeli ndani ya maji.

## Hatua ya 2

- Achia kitu kinachoelea kwa mkono mmoja na punga mkono wako nje ya maji.
- Piga kelele za kuomba msaada!

## Burudika!

- Wafanye wanafunzi washikilie kitu kinachoelea majini.
- Washawishi wanafunzi wapige miguu kwa nguvu na wajaribu kukitoa kitu kinachoelea nje ya maji.
- Watake wanafunzi wageuke / wazinguuke kila upande

## Kuokoa wengine


Muda: dakika 15

Uokoaji wa kufikia

Kina cha maji: kifuani

Uokoaji wa kufikia hutumika iwapo mtu aliye matatizoni yupo karibu na nchi kavu. Ni salama kwa sababu muokoaji halazimiki kuingia kwenye maji.

Lengo: Kuelewa kanuni za msingi za uokoaji wa kufikia.  
 Msaada: Wanafunzi wajifunze wenyewe bila ya kusaidiwa.



## Hاتua ya 1

- Ombo msaada!
- Zungumza na mtu aliye matatizoni huku ukitafuta kifaa cha msaada, kama fimbo ndefu au kipande kirefu cha kitambaa.
- Lala chini, ukimtazama anaehitaji msaada.

## Hاتua ya 2

- Ikiwezekana, shikilia kitu ili usiburuzwe majini.
- Nyoosha kifaa cha uokozi, ukikisogezza mbele ya anaehitaji msaada.
- Mwambie akishikilie kifaa cha uokozi, na wavute ukingoni.

## Mapitio na mazoezi

Muda: dakika 15

- Pitia Somo la 6.
- Wanafunzi watumie muda kufanya mazoezi ya vipengele wanavyohitaji.

## Somo la 7

### Matokeo ya somo

- Kuweza kuonyesha uingiaji na utokaji salama bila kusaidiwa.
- Kuweza kuruka na kuchupa kwenye maji ya kifua na kitu kinachoelea.
- Kuweza kuruka ikisha kugusa chini na kutoa pumzi kidogo kidogo.
- Kuweza kuelelea kwa mbele kwasekunde 10 na kurudia tena kusimama na kitu kinachoelea
- Kuweza kusukuma na kuelea kwa kulalia tumbo na kitu kinachoelea.
- Kuweza kupiga miguu kwa kulalia tumbo kwa sekunde 10 na kitu kinachoelea.
- Kuweza kupiga kasia kwenye maji kwa mikono na miguu kwa sekunde 20 huku wakishikilia kitu kinachoelea.
- Kufahamu mambo ya msingi ya uokozi wa kurusha.

### Vifaa

- Fimbo ndefu.
- Vitu vinavyoolea.
- Kamba.

## Weka sheria


## Muda: dakika 2

Weka kanuni za tabia.


## Kuingia/kutoka

## Muda: dakika 3

Kuingia upande wenyе kina:  
hutumika kuingia kwenye  
upande wa maji yenye kina.



Kuingia kwenye mteremko:  
hutumika kuingia kwenye  
maji yenye mteremko.



Kutoka kwenye upande wenyе kina:  
hutumika kutoka kwenye maji  
yenye kina.

## Mwendo

## Muda: dakika 5

Kuruka majini

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kuruka na kuchupa kwenye maji ya kifuani na kitu kinachoelea.  
 Msaada: Wanafunzi kushikilia kitu kinachoelea kwa mikono miwili. Wakizoea kwa mkono mmoja.




## Hatua ya 1

- Shikilia kitu kinachoelea kwa mikono miwili.
- Chuchumaa kama unakaa.

Kuchupa majini

Kina cha maji: kiuno hadi kifua



## Hatua ya 1

- Nyanya uguu mmoja na simama kwa uguu mmoja.

- Wanafunzi wakijiamini zaidi, zidisha kina cha maji taratibu kutoka maji ya kiunoni hadi maji ya kifuani.
- Wahimize wanafunzi kusogea ndani ya maji kuelekea pande tofauti.

## Hatua ya 2

- Jaribu kuchupa uliposimama kwa uguu mmoja.



## Kupumua

Muda: dakika 5

Zamisha mwili kwenye maji na gusa chini mara kadhaa.


**Kina cha maji: kifuani**

- Lengo: Kuweza kuruka na kuzama kwenye maji na kugusa chini huku ukitoa pumzi kidogo kidogo.
- Msaada: Wanafunzi kutengeneza duara na kushikana mikono kwa ajili ya kusaidiana au na rafiki.




### Hatua ya 1

- Vuta pumzi ndefu.



### Hatua ya 2

- Ingiza mwili na kichwa chako kwenye maji.
- Jaribu kugusa chini.
- Toa pumzi kidogo kidogo hadi ziishe.



### Hatua ya 3

- Hewa yote ikishakutoka, toa kichwa chako kwenye maji na vuta pumzi.

### Hatua ya 4

- Ingiza mwili na kichwa chako kwenye maji.
- Jaribu kugusa chini.
- Toa pumzi kidogo kidogo hadi ziishe.
- Rudia hatua hizi mara kadhaa.



## Kuelea

Muda: dakika15

Kuelea kifudi fudi na kitu kinachoelea

Kima cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kuelea kifudi fudi kwa sekunde 10 na kurudia kusimama na kitu kinachoelea.
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mikono miwili.



## Hatua ya 1

- Weka kitu chenye kuelea mbele juu ya maji mbele yako
- Nyoosha mikono
- Vuta pumzi nyngi.



## Hatua ya 2

## Hatua ya 2

- Tia uso wako kwenye maji.
- Nyoosha miguu nyuma yako.

Kupumua:

Washajihishe wanafunzi wapuliza kwenye maji wakati nyuso zao wamewe kwenye maji.

- Ukiishiwa pumzi sageza magoti yako kifuani, nyanya kichwa juu, sukuma kwa mikono yako na tuisha miguu chini.




## Kusukuma na kueleaa

Muda: dakika15

Kusukuma na kunyinyirika na kitu kinachoelea

**Kina cha maji: kiunoni**

- Lengo: Kuweza kusukuma na kunyinyirika kifudi fudina kitu kinachoelea.
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mikono miwili.



### Hatua ya 1

- Simama kwenye maji ya kiunoni na inama mbele kuanzia kiunoni.
- Weka kitu chenye kueleaa juu ya maji
- Nyoosha mikono yako mbele.
- Vutapumzi nyingi
- Inamisha kichwa hadi uso uzame kwenye maji.

### Hatua ya 2

- Inama mbele na sukuma kwa vidole vyako hadi miguu ielee kwenye usawa wa maji.
- Kaa hivyo hadi mwili wako utaposimama au kuishiwa na pumzi.

**Kupumua:**

Wasajihishe wanafunzi wapuliza kwenye maji wakati nyuso zao wameweka kwenye maji.


## Kupiga miguu

Muda: dakika15

Piga miguu kwa mbele  
kwa kitu chenye kuelea

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kupiga miguu kwa mbele kwa sekunde 10 kwa kitu chenye kuelea
- Msaada: Mwanafunzi atashikilia kitu chenye kuelea kwa mikono miwili



## Hatua ya 1

- Simama kwenye maji ya kifuani na inama mbele kutokea kiunoni.
- Nyoosha mikono yako mbele.
- Inamisha kichwa hadi uso uzame kwenye maji.

## Hatua ya 2

- Piga miguu mmoja baada mwengine.
- Piga miguu kuanzia kiunoni.
- Nyoosha na legeza miguu yako.

## Kupumua:

- Washajihishe wanafunzi wapuliza kwenye maji wakati nyuso zao wameweka kwenye maji.



### Mikono na miguu

Muda: dakika 15

Mikono na miguu na kitu kinachoelea


Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kupiga mikono na miguu kwa sekunde 20 ukishikilia kitu kinachoelea.
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea, mkono wao ukiwa umenyooshwa.




#### Hatua ya 1

- Zamisha uso kwenye maji.



#### Hatua ya 2

- Nyoosha mkono wako mtupu na unyoooshe kadri uwezavyo.



#### Hatua ya 3

- Vuta mkono wako kueleakea kiwiliwili.

#### Hatua ya 4

- Piga miguu kwa wakati huo huo.
- Nyanya kichwa chako kupumua.
- Ukiweza kujiamini kufanya hilo, weka kitu kinachoelea mkono mwengine na rudia zote.

#### Kupumua:

- Wahimize wanafunzi kutoa pumzi kidogo kidogo huku uso ukiwa kwenye maji.
- Wahimize wanafunzi kupumua kwa kugeuza kichwa pembeni.

#### Mapigo:

- Ikiwa mwanafunzi anapata shida kutoa mikono yake nje, mwambie apige yakiwa ndani. ya maji na anyanyuwe uso wake kwa kupumua.

## Kuokoa wengine

Muda: dakika 15

### Uokoaji wa kurusha

Mara nyingi uzamaji hutokea karibu na pembezoni. Uokoaji wa kurusha hutumika pale mtu anapokuwa mbali mno kuweza kufanya uokoaji wa kufikia, lakini karibu nya kutosha kuweza

**Kina cha maji: kifuani**

- Lengo: Kuelewa kanuni za msingi za uokoaji wa kurusha.
- Msaada: Wanafunzi kufanya zoezi bila kusaidiwa.

Waweke wanafunzi wawili wawili, mmoja akisimama kwenye maji ya kifua akijifanya kuwa yupo matatizoni na mwengine akisimama pembezoni.

### Na kitu kinachoelea



### Hatua ya 1

- Omba msada!
- Zungumza na aliye matatizoni – mwambie kuwa utamrushia kitu akishikilie.

### Na kamba



### Hatua ya 1

- Zungusha kamba mkononi, hakikisha kuwa maduara ni ukubwa unaofanana na hayajazongana.
- Hakikisha kamba imeshikiliwa vizuri kwenye mkono usiotumika kurushia.

### Hatua ya 2

- Rusha kamba itue juu ya mtu aliye matatizoni.
- Mlete mtu huyo ukingoni kwa kuivuta kamba taratibu na kwa uhakika.
- Kaa mbali na kingo wakati wa kuvuta kamba.

### Burudika!

- Fanyeni mazoezi ya shabaha kwa kuwasimamisha wanafunzi kwenye ukingo na kurusha vyombo vyao vinavyoolea au kamba kwenye shabaha majini. Angalia nani atakaribia shabaha zaidi!
- Shindanisha kuona nani atamuokoa mwenziwe haraka zaidi.

## Somo la 8

### Matokeo ya somo

- Kuweza kuingia na kutoka salama majini kwa kusaidiwa.
- Kuweza kuruka juu na baadae kuzama kwenye maji na kukaa chini huku ukitoa pumzi kidogo kidogo, na kurudia mara kadhaa.
- Kuweza kuelea chali kwa sekunde 10 na kitu kinachoelea na kurudia kusimama.
- Kuweza kusukuma na kuelea chali na kitu kinachoelea.
- Kuweza kupiga miguu chali kwa sekunde 10 na kitu kinachoelea.
- Kuweza kusogea ndani ya maji kwa kutumia mikono na miguu na kitu kinachoelea.
- Kuweza kubiruka kutoka chali hadi kifudi fudi na kitu kinachoelea.

### Vifaa

- Fimbo ndefu.
- Vyombo vinavyoolea.
- Kamba.

## Weka sheria


## Muda: dakika 2

Weka kanuni za tabia.

## Kuingia/kutoka

## Muda: dakika 3


Kuingia upande wenyе kina:  
hutumika kuingia kwenye  
upande wa maji yenye kina.



Kuingia kwenye mteremko:  
hutumika kuingia kwenye  
maji yenye mteremko.



Kutoka kwenye upande wenyе kina:  
hutumika kutoka kwenye maji  
yenye kina.




## Kupumua

Muda: dakika 10

Kuzama kwenye maji na  
kukaa chini


Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kuruka mfululizo na baadae kuzama kwenye maji na kukaa chini huku ukitoa pumzi kidogo kidogo.
- Msaada: Wanafunzi wasimame kwenye umbo la duara wakishikana mikono na rafiki zao.



### Hatua ya 1

- Vuta pumzi nyingi.



### Hatua ya 2

- Zamisha mwili na kichwa chako kwenye maji na kaa kitako chini.
- Toa pumzi kidogo kidogo mpaka ziishe.



### Hatua ya 3

- Hewa yote ikitoka, toa kichwa chako kwenye maji na vuta pumzi.

### Hatua ya 4

- Zamisha mwili na kichwa chako kwenye maji na kaa kitako chini.
- Toa pumzi kidogo kidogo mpaka ziishe.
- Rudia zoezi hili mara kadhaa.


## Kuelea

Muda: dakika 10

Kuelea chali na kitu kinachoelea

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kuelea chali kwa sekunde 10 na kitu kinachoelea na baada ya hapo kusimama.
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea karibu na kifua.



## Hاتua ya 1

- Lala chali kwenye maji.
- Laza kichwa chako na angalia juu.
- Hakikisha masikio yako ndani ya maji.

## Hاتua ya 2

- Sukuma tumbo lako juu usawa wa maji.
- Nyoosha miguu yako.
- Baada ya sekunde 10, pinda magoti na weka miguu chini kwenye mchanga usimame tena.


## Sukuma na nyenyereka

Muda: dakika15

Sukuma na nyinyirika chali na  
kitu kinachoelea


Kina cha maji: kiuno

- Lengo: Kuweza kusukuma na kunyiririka chali na kitu kinachoelea.
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea karibu na kifua kwa mikono miwili.



### Hatua ya 1

- Simama kwenye maji ya kiuno.
- Chutama kiasi cha kuwa mabega yako yako ndani ya maji.



### Hatua ya 2

- Lalia mgongo kwenye maji na sukuma kwa nguvu kwa vidole hadi mwili wako usogee ndani ya maji na miguu yako ielee juu ya maji.

### Hatua ya 3

- Nyoosha miguu yako.
- Tulia hadi mwili wako utakaposimama


## Kupiga

Muda: dakika15

Kupiga miguu chali na kitu kinachoelea

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kupiga miguu chali kwa sekunde 10 na kitu kinachoelea .
- Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea karibu na kifua kwa mikono miwili.



## Hاتua ya1

- Pinda nyuma.
- Sukuma miguu yako kutoka kwenye mchanga.
- Sukuma tumbo lako juu.
- Laza kichwa chako hadi masikio yawe majini.

## Hاتua ya 2

- Piga miguu yako mmoja baada mwengine.
- Piga miguu kuanzia kiunoni.
- Nyoosha na legeza miguu yako.
- Weka magoti yako chini ya maji.

## Miguu na mikono



Muda: dakika 20

Miguu na mikono na kifaa kinachoelea

Kina cha maji: kifuani


Lengo: Kuweza kupiga miguu na mikono kwa sekunde 20 huku ukishikilia kitu kinachoelea.

Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mkono mmoja, na mkono mwengine unyooshwe.



## Hatua ya 1

- Ingiza uso wako kwenye maji.



## Hatua ya 3

- Vuta nyuma mkono kufuata mwili wako.

## Hatua ya 2

- Nyoosha mbele mbali uwezavyo mkono wako mtupu.



## Hatua ya 4

- Piga miguu wakati huo huo.
- Ukishajiamini kufanya hili, weka kifaa kinachoelea kwenye mkono mwengine na rudia hatua hizo.

## Kupumua:

- Wahimize wanafunzi kutoa pumzi kidogo kidogo huku uso ukiwa kwenye maji.
- Wahimize wanafunzi kupumua kwa kugeuza kichwa pembeni.

## Mapigo:

- Ikiwa mwanafunzi anapata shida kutoa mikono yake nje, mwambie apige yakiwa ndani. ya maji na anyanyuwe uso wake kwa kupumua.

## Kujiokoa




Muda: dakika 15

Kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali

**Kina cha maji: kifuani**

Kuweza kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali kunawasaidia wanafunzi kupumzika iwapo watachoka wakiwa wanaogelea.

- Lengo: Kuweza kugeuka kutoka chali hadi kifudi fudi na kitu kinachoelea.  
 Msaada: Wanafunzi washikilie kitu kinachoelea kwa mkono mmoja.



### Hatua ya 1

- Elea kifudi fudi majini.
- Sukuma ndani ya maji kwa mkono mmoja.



### Hatua ya 2

- Geuza mwili wako wote kuelekea mkono unaosukuma ndani ya maji.
- Geuka hadi ulale chali.

### Hatua ya 3

- Legeza mwili wako ndani ya maji.
- Elea chali.
- Vuta pumzi taratibu bila papara.

## Somo la 9– Mazoezi

Muda: dakika 90

**M pangilio****Weka sheria**

Weka kanuni za tabia.

**Kuingia/kutoka**

Wanafunzi waweze kuonyesha kuingia/kutoka salama.

**Mwendo**

Wanafunzi waweze kusogea ndani ya maji kwa kusaidiwa na vitu vinavyoolea.

**Kupumua**

Wanafunzi wazowee kuzama ndani ya maji, kutoa pumzi nje, kuibuka na kupumua.

**Mapigo****Kuelea**

Wanafunzi waweze kuelea kifudi fudi na chali kwa sekunde 10 na kifaa kinachoelea.

**Kusukuma na kuelea**

Wanafunzi waweze kujisukuma na kunyenyereka kifudi fudi na chali na kifaa kinachoelea.

**Kupiga miguu**

Wanafunzi waweze kupiga miguu kifudi fudi na chali kwa sekunde 10 na kitu kinachoelea.

**Mikono**

Wanafunzi waweze kupiga mikono na kitu kinachoelea.

**Msaada****Kujisaidia**

Wanafunzi waweze kuelea wima kwa kutumia miguu pekee huku wakishikilia kifaa kinachoelea.

Wanafunzi waweze kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali na kifaa kinachoelea.

**Kuwaokoa wengine**

Wanafunzi waelewe kanuni za msingi za uokoaji wa kufikia na kurusha.

## Somo la 10

### Matokeo ya somo

- Kuweza kuingia na kutoka majini salama bila kusaidiwa.
- Kuweza kutembea na kukimbia kwenye maji ya kifua bila ya kusaidiwa.
- Kuweza kupiga mikono ndani ya maji bila ya kusaidiwa.
- Kuweza kuelewa wima kwa kutumia miguu na mikono, na bila ya kusaidiwa.
- Kuelewa kanuni za msingi za uokoaji wa kukwamua.

### Vifaa

- Fimbo ndefu.


### Weka sheria

Weka kanuni za adabu.

### Muda: dakika 2

### Kuingia/kutoka

Kuingia kwa upande ulio juu:  
inatumika kuingia kwenye  
maji kutokea upande ulio  
juu.




### Muda: dakika 3

Kuingia kwa upande wenye muinuko:  
inatumika kuingia kwenye  
maji kutokea upande wenye  
muinuko.



Kutoka kutokea upande ulio juu:  
inatumika kutoka kwenye maji  
kutokea upande ulio juu.



## Mwendo


## Muda: dakika 10

Kutembea na kukimbia majini

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kutembea na kukimbia kwenye maji ya kifua bila ya kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi wajifunze bila ya kusaidiwa.

- Wapange wanafunzi sambamba na ukingo kwenye maji ya kifua.
- Waongoze wanafunzi watembee sambamba na ukingo.



### Hatua ya 1

- Unda mstari na tembea mbele pole pole, ukimfuata mtu aliyepo mbele yako.

- Wanafunzi wakijiamini zaidi, ongeza kasi ya mwendo na kina cha maji.
- Muelekeze mwanafunzi aliyepo mbele kubadili muelekeo.

## Mikono

## Muda: dakika 15

Kupiga mikono ukitembea

Kina cha maji: kifuani

Lengo: Kuweza kupiga mikono kwenye maji bila ya kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi kujaribu wenyewe bila kusaidiwa.



## Hatua ya 1

- Vuta pumzi myingi.
- Ingiza uso wako majini na tembea mbele taratibu ndani ya maji.
- Tembea kwenye maji.
- Vidole vyako viweke pamoja.
- Nyoosha mkono wako na usogeze mbele kadri uvezavyo.

## Hatua ya 2

- Vuta mkono wako kiwiliwilini kwako.
- Sukuma maji nyuma yako.
- Toa mikono yako nnje / juu ya maji ukiwa unarejesha kuvuta maji.
- Badilisha mikono.
- Rejea
- Geuza kichwa chako ubavuni kwa kupumua

## Kupumua:

- Wahimize wanafunzi kutoa pumzi kidogo kidogo huku uso ukiwa kwenye maji.
- Wahimize wanafunzi kupumua kwa kugeuza kichwa pembeni.

## Mapigo:

- Ikiwa mwanafunzi anapata shida kutoa mikono yake nje, mwambie apige yakiwa ndani. ya maji na anyanyuwe uso wake kwa kupumua.

## Kujiokoa

Muda: dakika 20

Kuelea wima

Kuelea wima ni mbinu ya kuogelea inayomruhusu mtu kuweka kichwa nje ya maji na kuomba msaada kwa sauti.

Muogeleaji hukaa hapo hapo kwenye maji.

Kina cha maji: juu ya kifua

Lengo: Kuweza kuelea wima kwa mikono na miguu.

Msaada: Wanafunzi wafanye hivyo wenywewe bila kusaidiwa.

Wanafunzi wasiokuwa na uzoefu wanawenza kupata tabu kujifunza mbinu bila ya kusaidiwa. Iwapo watapata tabu, tumia vitu vinavyoelea kwa kuwasaidia.



## Hatua ya 1

- Weka kichwa chako juu.
- Nyoosha mikono yako pembeni ndani ya maji.
- Sukuma mikono yako mbele na nyuma ndani ya maji.

## Hatua ya 2

- Bakia ukiwa unaelea wima.
- Sukuma miguu yako nyuma na mbele kama unaendesha baiskeli ndani ya maji.

## Burudika!

- Wafanye wanafunzi wanyooshe mkono mmoja juu ya maji, kuupunga na kuomba msaada!

## Kuwaokoa wengine

Muda: dakika 20

### Uokoaji wa kukwamua

Kina cha maji: kifuanini

Uokoaji wa kukwamua unatumika kumsogelea karibu mtu anaehitaji msaada, huku ukigusa chini. Itumike pale tu ambapo hali ya maji haimuweki muokoaji kwenye hatari.

Lengo: Kuelewa kanuni za msingi za uokozi wa kukwamua.  
 Msaada: Wanafunzi wafanye mbinu hiyo bila ya kusaidiwa.



### Hatua ya 1

- Kuwa makini wakati unamuangalia majeruhi.



### Hatua ya 3

- Mpe ncha moja ya jiti

### Hatua ya 2

- ingia kwenye maji kwa makini ukiwa umechukuwa jiti, angalia kina cha maji pamoja na kumuangalia mtu unaemfuata



### Hatua ya 4

- Msaidie kumtowa nnje ya maji.

## Mapitio na mazoezi

Muda: dakika 20

- Pitia Somo la 10.
- Wanafunzi watumie muda kufanya mazoezi ya mbinu walizojifunza.

## Somo la 11

### Matokeo ya mafunzo

- Kuweza kuingia na kutoka salama bila kusaidiwa.
- Kuweza kuruka na kuchupa kwenye maji ya kifuanini bila ya kusaidiwa.
- Kuweza kuelelea kifudi fudi kwa sekunde 10 bila kusaidiwa.
- Kuweza kujisukuma na kunyinyirika kifudi fudi bila kusaidiwa.
- Kuweza kupiga miguu kifudi fudikwa sekunde 10 bila ya kusaidiwa.
- Kuweza kuogelea mita 10 kwa mikono na miguu bila kusaidiwa, kupumua kwa pembedi.

### Vifaa

- Fimbo ndefu.


## Weka sheria

Weka kanuni za tabia.

## Muda: dakika 2

### Kuingia/kutoka


Kuingia upande wenyne kina:  
hutumika kuingia kwenye  
upande wa maji yenye kina.



Kuingia kwenye mteremko:  
hutumika kuingia kwenye  
maji yenye mteremko.



Kutoka kwenye upande wenyne kina:  
hutumika kutoka kwenye maji  
yenye kina.



## Muda: dakika 3

## Mwendo

Muda: dakika 10

Chupa kwenye maji

Kina cha maji: kifuani

- Lengo: Kuweza kuruka na kuchupa kwenye maji ya kifua bila ya kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi wafanya hivyo bila ya kusaidiwa.




## Hatua ya 1

- Chuchumaa kama unataka kukaa.

Kuchupa majini

Kina cha maji: kifuani



## Hatua ya 1

- Nyanyua mguu mmoja na jaribu kusimama kwa mguu mmoja.

- Wanafunzi wakijiamini zaidi, ongeza kina cha maji kidogo kidogo kutoka kiunoni hadi kifuani.
- Rudia tena kwa kusogea mbele, nyuma na pembedi ndani ya maji.

## Hatua ya 2



- Jaribu kuchupa hapo ulipo simama.

**Kuelea*****Muda: dakika***

Kuelea kifudi fudi

Kina cha maji: kifuani

Lengo: Kuweza kuelea kifudi fudi kwa sekunde 10 bila kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi kutumia mwalimu au wenzao kwa msaada ikilazimu.

**Hatua ya 1**

- Nyoosha mikono yako kwa pemberi.
- Zuwia pumzi.

**Hatua ya 2**

- Tia uso wako kwenye maji.
- Nyoosha miguu yako nyuma yako.

**Hatua ya 3**

- Pumzi zikikuishia nanyua kichwa juu, sukuma chini kwa mikono yako, elekeza magoti yako kwenye kifua chako na weka miguu yako chini.


## Sukuma na nyinyirika

Muda: dakika15

Kusukuma na kunyinyirika kifudi fudi

Kina cha maji: Kiunoni

Lengo: Kuweza kusukuma na kunyenyereka kifudi fudi bila ya kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi watumie mwalimu au mwenza kusaidiwa ikihitajika.



## Hatua ya 1

- Simama kwenye maji ya kiuno.
- Nyoosha mikono juu ya kichwa chako, na ikutanishe pamoja.



## Hatua ya 2

- Inamia mbele na sukuma kwa nguvu kwa vidole vyako ili kiwiliwili chako kisogee ndani ya maji na miguu yako ielee majini.
- Nyoosha miguu yako.
- Kaa hivyo hadi mwili utapo simama au kuishiwa na pumzi.

## Hatua ya 3

- Ukiishiwa na pumzi sogeza magoti yako kifuani, nyanyua kichwa chako, sukuma chini kwa mikono yako na tuisha miguu yako chini.



## Kupiga miguu

Muda: dakika 15

Kupiga miguu

Kina cha maji: Kiunoni

Lengo: Kuweza kupiga miguu kwa sekunde 10 bila kusaidiwa.  
 Msaada: Ikilazimika mwalimu anaweza kutoa mwega chini ya mabega.



## Hatua ya 1

- Simama kwenye maji ya nyonga na inama kidogo kuelekea mbele
- Nyoosha mikono yako juu ya kichwa na ikutanishe pamoja.
- Vuta pumzi nyingi.
- Ingiza uso wako majini.
- Sukuma vidole vyako kutoka mchangani.

## Hatua ya 2

- Piga miguu yako mmoja baada ya mwengine.
- Piga miguu kutokea kiunoni.
- Nyoosha na legeza miguu yako.



## Miguu na mikono

Muda: dakika 30

Miguu na mikono


Kima cha maji: kifuani

Lengo: Kujaribu kuogelea kwa kutumia miguu na mikono.  
 Msaada: Wanafunzi wajifunze mbinu bila ya kusaidiwa.



## Hatua ya 1

- Ingiza uso wako ndani ya maji.



## Hatua ya 2

- Nyoosha mkono wako na ukamate mbele mbali uwezavyo kwa mkono wako.



## Hatua ya 3

- Rudisha mkono wako kwenye mwili wako.
- Sukuma maji nyuma yako.
- Toa mkono kwenye maji kiunoni mwako.

- Wanafunzi huenda wakaweza masafa mafupi tu kabla kuweka miguu yao chini.
- Wahimize kufanya mazoezi na waongezee masafa.
- Wahimize wanafunzi kupumua kwa kugeuza vichwa vyao pembedi.

Mapigo:

- Ikiwa mwanafunzi anapata shida kutoa mikono yake nje, mwambie apige yakiwa ndani.

## Hatua ya 4

- Piga miguu wakati huo huo.

### Somo la 12

#### Matokeo ya somo

- Kuweza kuingia na kutoka majini kwa salama bila kusaidiwa.
- Kuweza kuelea chali kwa sekunde 30 bila kusaidiwa.
- Kuweza kufanya mbinu ya kusukuma na kuelea chali bila kusaidiwa
- Kuweza kupiga miguu chali kwa sekunde 10 bila kusaidiwa.
- Kuogelea kwa mita 25 au sekunde 45 kwa kutumia miguu na mikono, bila kusaidiwa.
- Kuweza kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali bila kusaidiwa.

#### Vifaa

Hamna.

#### Weka sheria

#### Muda: dakika 2



Weka kanuni za nidhamu.

**Kuingia/kutoka****Muda: dakika 3****Uingiaji magamaga**


Inatumika kuingia haraka katika maji yeny kina kirefu yasiyo na vitu visivyoonekana.

**Kina cha maji: urefu wa mtu na sentimita 50**


**Tanabahi:** Fundisha uingiaji magamaga pale tu eneo la kufundishia lina kina kirefu na halina vitu chini ya maji. Iwapo hakuna maji ya kina kirefu, basi fundisha uingiaji wa mteremko au wa upande wa kina.

**Hatua ya 1**

- Ukiwa umesimama, miguu ikiwa imetanuliwa kidogo, piga hatua moja kubwa juu ya maji.

**Hatua ya 2****Hatua ya 2**

- Kunja mguu wako wa mbele na nyosha mikono yako upande usawa wa mabega.



- Inama mbele kidogo.

**Hatua ya 4**

- Shusha mikono yako chini, mikono yako itapogusa maji.
- Funga miguu yako na weka kichwa chako juu ya maji.



## Kuelea

Muda: dakika 5

Kuelea chali

Kiwango cha maji: Kifuani

Lengo: Kuweza kuelea chali kwa sekunde 30 bila kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi wajaribu mbinu hiyo kwa zamu. Ikilazimu, mwalimu anaweza kutoa mwega chini ya mabega.



## Hatua ya 1

- Nyoosha mikono yako kwa upande.
- Lala chali kwenye maji.
- Laza kichwa chako ili masikio yaye ndani ya maji.

## Hatua ya 2

- Nyanyua tumbo lako juu kwenye usawa wa maji.
- Nyoosha miguu yako.



## Sukuma na nyinyirika

Muda: dakika 15

Sukuma na ninyirika chali

Kina cha maji: kiunoni

Lengo: Kuweza kusukuma na kunyinyirika chali bila kusaidiwa.  
 Msaada: Wnafunzi wanajaribu mbinu kwa zamu. Ikilazimu, mwalimu anaweza kutoa mwega chini ya mabega.




## Hatua ya 1

- Simama kwenye maji hadi kiunoni.
- Nyoosha mikono yako chini.

## Hatua ya 2

- Lalia mgongo kwa kusukuma na vidole vyako vya mguu, ili mwili wako ulalie maji na nyayo zako zielea juu ya maji.
- Nyoosha miguu yako.
- Kaa hivyo hadi mwili wako utakaposimama.



Ikiwa wanafunzi wanaweza kusukuma na kunyenyeraka mikono yao ikiwa chini, jaribu tena na mikono yao imenyooshwa juu kichwani.


## Kupiga miguu

Muda: dakika 15

Kupiga miguu mgongo

Kina cha maji: kifuani

Lengo: Kuweza kupiga miguu chali kwa sekunde 10 bila kusaidiwa.  
 Msaada: Wanafunzi wajaribu mbinu kwa zamu. Ikilazimu, mwalimu anaweza kutoa mwega chini ya mabega.



## Hatua ya 1


- Sukuma miguu yako juu ya mchanga.
- Sukuma tumbo lako juu.
- Weka mikono sambamba na kiwiliwili.
- Laza kichwa chako ili masikio yako yawemo ndani ya maji.

Kupiga mikono ukiwa chali:

- Ikiwa mwanafunzi anaweza kupiga miguu akiwa chali, wahimize kutumia mikono kujisogeza ndani ya maji.
- Zungusha mikono kwa umbo la mviringo, ukisukuma maji chini ya kiwiliwili.

## Hatua ya 2

- Piga miguu mmoja baada ya mwengine.
- Piga miguu kuanzia kiunoni.
- Nyoosha na legeza miguu yako.
- Jaribu kuweka magoti yako ndani ya maji.





## Miguu na mikono

Muda: dakika 20

Miguu na mikono kifudi fudi

Kina cha maji: kifuani

Lengo: Jaribu kuogelea kwa kutumia miguu na mikono bila ya kusaidiwa  
 Msaada: Wanafunzi wafanye hivyo wenyewe bila kusaidiwa.




## Hatua ya 1

- Ingiza uso kwenye maji
- Peleka kisugudi chako juu nje ya maji.



## Hatua ya 2

- Nyoosha mkono wako na upeleke mbali hadi utakapofika mkono wako.



## Hatua ya 3

- Vuta nyuma mkono wako kuelekea kiwiliwili chako.
- Utoe mkono wako nje ya maji, usawa wa kiuno chako.

- Wanafunzi huenda wakawenza umbali mfupi tu kabla ya kuweka miguu yao chini.
- Wahimize kufanya mazoezi na kuongeza umbali kidogo kidogo.

## Hatua ya 4

- Piga miguu wakati huo huo

## Kujiokoa

Muda: dakika 20


Kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali

Kina cha maji: Kifuani

Kuweka kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali kunawasaidia wanafunzi kupumzika chali iwapo watachoka wakiwa wanaogelea.


Lengo: Kuweza kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali bila kusaidiwa.

Msaadat: Wanafunzi wajaribu mbinu hiyo kwa zamu. Inapohitajika, mwalimu anaweza kutoa mwega chini ya mabega.



### Hatua ya 1

- Elea kifudi fudi ndani ya maji. Sukuma chini ndani ya maji kwa mkono.



### Hatua ya 2

- Geuza mwili wako mzima upande wa mkono unaosukuma ndani ya maji.
- Geuka hadi ulalie mgongo wako.

### Hatua ya 3

- Legeza mwili wako ndani ya maji.
- Elea chali.
- Vuta pumzi taratibu bila papara.

**Somo la 13 and 14 - Mazoezi****Muda: dakika 90****Muelekeo****Weka sheria**

Weka kanuni za tabia.

**Kuingia/Kutoka**

Wanafunzi wanapaswa kuweza kuonyesha uingiaji/utokaji salama.

**Mwendo**

Wanafunzi waweze kutembea ndani ya maji bila ya kusaidiwa.

**Mapigo****Kuelea**

Wanafunzi waweze kuelea kifudi fudi kwa sekunde 10 na chali kwa sekunde 30 bila ya kusaidiwa.

**Kusukuma na Kuelea**

Wanafunzi waweze kusukuma na kuelea kifudi fudi na chali bila kusaidiwa.

**Kupiga mateke**

Wanafunzi waweze kupiga mateke kifudi fudi na chali kwa walau sekunde 10 bila ya kusaidiwa.

**Miguu na Mikono**

Wanafunzi waweze kutumia miguu na mikono yao na kuogelea mita 25 bila msaada.

**Msaada****Kujiokoa**

Wanafunzi waweze kuonyesha kupiga mikono bila kusaidiwa.

Wanafunzi waweze kugeuka kutoka kifudi fudi hadi chali bila ya kusaidiwa.

**Kuwaokoa wengine**

Wanafunzi waelewe kanuni za msingi za uokozi wa kukwamua.

## Somo la 15

### Matokeo ya somo

- Wanafunzi wote wakamilishe tathmini

### Vifaa

- Fomu za usajili na za tathmini
- Vifaavya uokozi

## Weka sheria

Weka kanuni za

## Mazoezi

Kwa nusu ya kwanza ya kipindi, fanya zoezi kwa kitendo chochote kwakukamilisha vigezo vya tathmini.

## Tathmini

- Kila mwanafunzi atathminiwe peke yake.
- Wanafunzi waliokuwa hawatathminiwi kwa wakati ule, wasubiri mahali salama nje ya maji.
- Ili kukamilisha kwa mafanikio darasa, mwanafunzi anapaswa:
  - kuogelea kifudi fudi au chali kwa mita 25
  - kuelea chali kwa sekunde 30
  - kuogelea na kifaa kinachoelea
  - waonyeshe uokoaji wowote wa nchi kavu.
- Weka alama ya ‘kufaulu’ kwa kujaza alama ya ndio kwenye kiboksi husika kwenye fomu ya Usajili na ya tathmini.

## 2.8 Michezo na Vitendo

### 2.8 Michezo na vitendo

Michezo na vitendo vinaweza kutumika wakati wowote kufanyia mazoezi ya mbinu ulizofundishwa kwenye muongozo huu. Ina faida hususan kwa kufundishia watoto wadogo.

Michezo iwe na shauku yake na kufurahiwa lakini ni muhimu kwa mwalimu kuwa mdhibiti wa michezo hiyo wakati wote.

Michezo hii inaweza kubadilishwa kuendana na mazingira yako. Ukipuni mchezo mwengine, usisahau kuuandika ili usisahau!



#### Kuingia/Kutoka

Kusaka vitu macho yakiwa yamefumbwa

Vifaa	<ul style="list-style-type: none"><li>Vitu vya kuwafumbia macho wanafunzi.</li><li>Vitu vidogo vidogo kama chupa za plastiki.</li><li>Fimbo ndefu.</li></ul>
Lengo	<p>Kufanya mazoezi ya kutafuta vitu vya hatari kwa kutumia fimbo.</p> <ol style="list-style-type: none"><li>Tenga eneo la kufundishia mchangani.</li><li>Wagawe wanafunzi wawili wawili.</li><li>Wapange wanafunzi sambamba na mpaka wa eneo la kufundishia.</li><li>Mfumbe macho mmoja ya wanafunzi kati ya kila wawili.</li><li>Weka vitu katika eneo lote la kufundishia.</li><li>Mwanafunzi aliyefumbwa macho atafute vitu vingi awezavyo kwa kutumia fimbo na maelezo ya mwenzake.</li><li>Wanafunzi wabadilishane zamu!</li></ol>
Ujuzi	Kutumia fimbo kutafuta vitu hatari majini na kuelewa umuhimu wake.
Mabadiliko	Hamna.

## 2.8 Michezo na vitendo

### Vitendo

#### Nimekwama mchangani

Vifaa	Hamna
Lengo	Kuwaongeza ujasiri wa kutembea ndani ya maji.
Maelezo	<ol style="list-style-type: none"><li>Chagua sehemu ya kufundishia kwenye maji ya kina kifupi.</li><li>Wachague wanafunzi wawili wawe 'wakamataji'.</li><li>Waambie wanafunzi wakimbie kimbie. Wakamatwa na 'wakamataji' wasimame tuli huku wakiwa wamefungua miguu yao.</li><li>Wanafunzi waliokamatwa wanaweza kukimbia tena pale tu mwanafunzi mwengine akipita katika miguu yao.</li><li>Mchezo utakwisha pale wanafunzi wote watakapokuwa wamesimama.</li><li>Badilisha 'wakamataji' na mcheze tena!</li></ol>
Ujuzi	Kukimbia na kutambaa ndani ya maji.
Mabadiliko	Wanagenzi: maji ya kwenye viwiko vya mguu. Ngazi ya kati: maji ya kwenye magoti. Ngazi ya juu: maji ya kwenye kifua.

#### Resi za kuruka na kuchupa

Vifaa	Vitu vinavyoolea (ikilazimu).
Lengo	Kuungeza ujasiri wa kutembea ndani ya maji.
Maelezo	<ol style="list-style-type: none"><li>Weka alama za kuanza na kumaliza kwa resi.</li><li>Wapange wanafunzi kwenye mstari wa kuanzia.</li><li>Watake wanafunzi waruke au wachupe haraka wawezavyo hadi mwisho.</li></ol>
Ujuzi	Kubalansi ndani ya maji. Kutembea ndani ya maji ya kifua.
Mabadiliko	Mwanagenzir: maji ya magoti Ngazi ya kati: maji ya kifua na kifaa kinachoelea Ngazi ya juu: maji ya kifua bila ya kifaa kinachoelea

#### Kuruka mbali zaidi

Vifaa	Vitu vinavyoolea (ikilazimu).
Lengo	Kuungeza ujasiri wa kutembea ndani ya maji.
Maelezo	<ol style="list-style-type: none"><li>Weka mstari wa kuanzia ndani ya maji.</li><li>Watake wanafunzi waruke mbali wawezavyo ndani ya maji</li><li>Angalia nani ataruka mbali zaidi!</li></ol>
Ujuzi	Kubalansi ndani ya maji. Kutembea ndani ya maji.
Mabadiliko	Mwanagenzi: maji ya magoti. Ngazi ya kati: maji ya kiuno na kifaa kinachoelea. Ngazi ya juu: maji ya kiuno bila ya kifaa kinachoelea.

## Pumzi

### Sema jina lako chini ya maji

Vifaa	Hakuna.
Lengo	Kuwaongeza ujasiri wa kuingiza mdomo majini na kupuliza chini ya maji.
Description	<ol style="list-style-type: none"> <li>Waweke wanafunzi katika pea (wawili wawili).</li> <li>Waingize kwa zamu nyuso zao kwenye maji na kusema majina yao.</li> <li>Muombe mwanafunzi anaesubiri zamu kuweka sikio kwenye maji na kusikiliza iwapo angemsikia akitaja jina lake.</li> </ol>
Ujuzi	Kupuliza chini ya maji. Kuweka uso na masikio chini ya maji.
Maendeleo	Mwanagenzi: Ingiza mdomo/uso tu kwenye maji. Ngazi ya kati: Ingiza kichwa chao chote kwenye maji. Ngazi ya juu: Ingiza kichwa chote chini ya maji na kaa chini kwenye maji.

### Resi za chupa za plastiki

Vifaa	Chupa za plastiki.
Lengo	Kuwaongeza ujasiri wa kuweka kidevu/mdomo kwenye maji na kutoa pumzi nje.
Maelezo	<ol style="list-style-type: none"> <li>Weka alama ya kuanza na kumalizia kwa resi.</li> <li>Muombe kila mwanafunzi aje na chupa ya plastiki.</li> <li>Waelekeze wanafunzi waweke chupa zao zikielea kwenye mstari wa kuanzia na wazipulize hadi mtari wa kunalizia resi.</li> </ol>
Ujuzi	Kupuliza pumzi nje wakiwa majini.
Mabadiliko	Hamna.

## Mapigo

### Sukuma na elea chini ya gongo

Vifaa	Gongo refu.
Lengo	Kuongeza ujasiri wa kusukuma na kunyinyirika.
Maelezo	<ol style="list-style-type: none"> <li>Kamata gongo refu kuwaelekea wanafunzi.</li> <li>Watake wanafunzi kusukuma miguu ardhini na kunyinyirika chini gongo.</li> </ol>
Ujuzi	Mazoezi ya kusukuma na kunyinyirika.

## 2.8 Michezo na vitendo

### Msaada

#### Kurusha kifimbo cha uokozi

Vifaa	Kifaa cha uokoaji kama kama debe au kamba
Lengo	Kufanya mazoezi ya uokoaji wa kurusha vifaa vyta uokoaji
Maelezo	<ol style="list-style-type: none"><li>Wagawe wanafunzi kwenye timu ndogo ndogo</li><li>Muweke mwanafunzi mmoja ufukweni na waliobakia kwenye mstari majini wakimuelekea mwenzao aliye ufukweni.</li><li>TMwanafunzi aliye ufukweni anakirusha kifaa kwa wa kwanza kwenye mstari ambae nae hupiga miguu kuelekea ukingo wa ufukwe.</li><li>Yule aliyeokolewa anarusha kifaa kwa wa pili kwenye mstari kama alivyorushiwa yeye hadi wanafunzi wote wakiwa 'wameokolewa.</li><li>Aliyekuwa ufukweni mwanzo kabisa anaweza kujinga na mstari baharini baada ya wenziwe kuokolewa ili nae apate kufanya mazoezi.</li></ol>
Ujuzi	Mafunzo ya kurusha kifaa cha uokoaji. Kuogelea na kifaa cha uokoaji. Kutoka salama baharini.
Mabadiliko	Zidisha umbali baina ya timu kwenye bahari na mrushaji wa kifaa. Tumia vifaa mbali mbali.



